SportPesa
TZS. 686,934,380
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



## Uchomaji moto misitu watajwa chanzo ukame

UKURASA 2



## Ronaldo hatarini kukosa Kombe la Dunia Qatar

UKURASA 21


# Nipashe

Jumanne Novemba 16, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580766

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Samia: Hii ndiyo hali mipaka yetu

UKURASA 2



Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama nchini, Rais Samia Suluhu Hassan (kulia), akiwa na Mkuu wa Majeshi (CDF), Venance Mabeyo, baada ya kufungua mkutano mkuu wa tano wa Makamanda wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) 2021, kujadili hali ya jeshi na taifa kwa ujumla katika kutekeleza majukumu yao, Lugalo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

KESI YA MBOWE

## Mawakili utetezi wakomaa shahidi aliyeingia na 'diary'

UKURASA 4





## Watuhumiwa wa ujambazi wakamatwa, mmoja auawa

UKURASA 3

MICHEZO SAMATTA NA SIMULIZI WANAJESHI KUMVAMIA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akizungumza na Balozi wa Heshima wa Tanzania nchini Singapore, TeoSieng Sengapore, alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Changi, Singapore. Mpango yupo Singapore kuhudhuria Mkutano wa Jukwaa la Majadiliano ya Kiuchumi. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Uchomaji moto misitu watajwa chanzo ukame

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Selemani Jafo, amesema uchomaji ovyo wa misitu umekuwa moja kati ya sababu zinazochangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa vyanzo vya maji nchini.

Jafo, alibainisha hayo jana jijini Dodoma wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mafanikio ya sekta ya muungano na mazingira katika kipindi cha miaka 60 ya Uhuru wa Tanganyika.

Alisema katika maeneo mengi hivi sasa kumekuwapo na matukio ya uchomaji misitu ovyo hali inayo tishia uharibifu wa vyanzo vya maji nchini.

"Uchomaji wa misitu umekuwa ukisababisha hata uharibifu wa vyanzo vya maji kwa mafano mkoa wa Morogoro ni mkoa ambao unategemewa sana kwa chakula na chanzo cha maji hata maji ya Mto Ruvu yanatoka Morogoro, ndiyo maana hata mkoa wa Dar es Saalam, maji yamekuwa ni shida sana kutokana na kuchoma msitu," alisema.

Aidha, alisema katika mkoa wa Morogoro miaka ya nyuma Bwawa la Mindu lilikuwa likitumika kama chanzo cha maji cha uhakika, lakini hivi sasa kutokana na uharibifu wa mazingira ikiwa ni pamoja na uchomaji wa misitu kumekuwapo na ukame mkubwa.

"Lakini hili tatizo la watu kuchoma misitu lina mambo mengi sana ikiwamo imani potofu kuna watu unakuta wanachoma msitu kwa kushindana ni nani moto wake utakwenda umbali mrefu na ambaye moto wake aliouwasha ukaenda mbali zaidi anaamini ataishi miaka mingi zaidi kama ambavyo moto huo umekwenda," alisema Jafo.

Katika hatua nyingine, Jafo alisema wizara nane, zimejipanga kushirikina kuishughulikia kero ya uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele za muziki kwenye kumbi za starehe na nyumba za ibada.

Jafo alisema pamoja na wizara hiyo kupata mafanikio katika maeneo mbalimbali toka Uhuru mwaka 1961, lakini bado yapo mambo ambayo yana kero kubwa zinazohitaji kuendelea kushughulikiwa.

Alisema, moja kati ya eneo ambalo bado ni kero hasa katika sekta ya mazingira ni suala la uchafuzi wa mazingira utokanao na makekele katika kumbi za starehe pamoja na nyumba za ibada.

"Watu bado wanapiga muziki kwa sauti za juu sana katika makazi ya watu, lakini katika nyumba za ibada bado changamoto hii ipo na kutokana na unyeti wa suala hili tumeanza kuwashirikisha viongozi wa dini ili kuona suala hili tunalimaliza vipi.

"Kule Dar es Saalam tayari Mkuu wa Mkoa, Amos Makala, aliitisha kikao cha viongozi wa dini ili kujadili suala hili maana yake haya ni maeneo ambayo yana unyeti wake lazima kwanza tukutane na viongozi hawa," alisisitiza Jafo.

Aidha, alisema uchafuzi wa mazingira utokanao na makelele umekuwa na madhara makubwa kama vile wajawazito kuharibika mimba, lakini watoto kupoteza usikivu.

"Madhara kama haya ya mimba kuharibika pamoja na watoto wadogo kupoteza usikivu ni kazi sana kumrudisha mtoto katika hali yake ya kawaida baada ya kupoteza uwezo wake wa kusikia, ndiyo maana hivi sasa tunakwenda kushirikiana na wizara nane kulikabili jambo hili," alisema.

Akizungumzia kuhusu upandaji miti alisema katika halmashauri zote nchini 184, kila moja imekuwa ikipanda miti milioni 1,500,000 kila mwaka.

"Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni ya upandaji miti kwa lengo la kurejesha uoto wa asili na kupunguza hali ya kuenea kwa jangwa na ukame ambapo kila halmashauri ya wilaya imeelekezwa kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka.

# Samia: Hii ndiyo hali mipaka yetu

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameyapongeza majeshi ya ulinzi na usalama kwa kufanya kazi nzuri katika ulinzi na usalama, akibainisha kuwa kwa sasa mipaka ya nchi iko shwari.

Amri Jeshi Mkuu huyo pia amezungumzia matukio ya kigaidi yaliyotokea katika mpaka wa Tanzania na Msumbiji mkoani Mtwara, akipongeza kazi nzuri iliyofanywa na majeshi kuwadhibiti wahalifu hao.

Alitoa pongezi hizo jana katika mkutano mkuu wa tano wa mwaka wa Mkuu wa Majeshi la Ulinzi na makamanda wa Jeshi la Wananchi, akisema jeshi limeendelea kuwa chombo kinachotumainiwa na wananchi na wamekuwa tayari kushirikiana nao kwa muda wote katika kuilinda nchi.

Alisema kuwa katika kipindi cha hivi karibuni hali ya ulinzi na usalama wa mipaka ya Tanzania hususani maeneo ya kusini ilihatarishwa na kuwapo kwa tishio la kundi la kigaidi katika Jimbo la Kabodelgado, Msumbiji linalopakana na Mkoa wa Mtwara na baadhi ya vijiji vyake vilivyokumbwa na matukio yaliyosababisha vifo, majeruhi na uharibifu wa mali.

Rais Samia alisema jeshi lilikabiliana na hali hiyo huku serikali ikipeleka vikosi maalum katika mpaka huo kwa ajili ya kuimarisha ulinzi na usalama, hali iliyosaidia kuleta utulivu na kurudisha shughuli za kiuchumi na kijamii katika eneo hilo pamoja na kupunguza hofu iliyokuwapo.

"Ninayasema haya kuwahakikishia wanajeshi popote mlipo serikali tupo, tunajua katika maeneo ya mipakani kuna changamoto kadhaa ikiwamo njia ya kufikia maadui walipo, usafiri, magari yenu pengine hayakidhi vigezo, yote tunayajua lakini niwaahidi tutajitahidi kukabiliana na changamoto zinazowakabili ili muweze kufanya kazi zenu vizuri zaidi.

"Ninaomba niwahakikishie kuwa serikali ina dhamira ya dhati ya kuendelea kuimarisha na kuliwezesha jeshi letu kukabiliana na changamoto mbalimbali za kiulinzi, muda mwingine mmekuwa mkilazimika kutekeleza majukumu yenu katika mazingira magumu na hatarishi zaidi, ninapenda kuwathibitishia kuwa serikali itahakikisha inatoa kila aina ya msaada ili muweze kutekeleza majukumu yenu kikamilifu," aliahidi Rais Samia.

Aliongeza kuwa pamoja na majukumu mengi ambayo jeshi linayatekeleza, jukumu la msingi linabaki kuwa la kulinda uhuru na mipaka ya nchi dhidi ya tishio la ndani na nje ya nchi kupitia nchi kavu, angani na majini, jukumu ambalo ni la kikatiba.



Alibainisha kuwa moja ya kusudi la msingi la kazi ya jeshi ni kulinda maslahi na uhuru wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo ni uhuru, haki za binadamu, undugu, mshikamano, umoja wa kitaifa na demokrasia.

Alisema ulinzi wa taifa una gharama kubwa na umuhimu wake hauwezi kulinganisha na kitu chochote.

Rais Samia alisema dunia kwa sasa inakabiliwa na tatizo jipya la kiusalama, hivyo akaliagiza jeshi na vyombo vingine vya usalama kujadili jambo hilo na kuimarisha weledi wao katika mapambano dhidi ya ugaidi ili kukabiliana nao kwa ukamilifu.

"Mapambano dhidi ya tishio la ugaidi si suala la vyombo vya ulinzi na usalama peke yenu, bali linahitaji ushirikiano kutoka taasisi mbalimbali vikiwamo vyombo vya habari na asasi za kiraia, zikiwa na jukumu la kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu wa amani na madhara ya kujihusisha na vitendo vya ugaidi.

"Katika tafakuri yenu muone jinsi ya kukaa na vyombo vingine lakini na taasisi kama vyombo vya habari, asasi za kiraia na waone jinsi watakavyoweza kutoa elimu kwa wananchi ili kujiepusha na ugaidi na kurahisisha kazi yenu kama walinzi wa usalama wa taifa letu," aliagiza.

Alisema amani na usalama ndio msingi wa maendeleo ya taifa, hivyo akaahidi kuendelea kufanya kila linalowezekana kulijenga jeshi ili liendane na wakati uliopo na lipambane na matishio ya kidunia yaliyopo.

Pia aliahidi kwa kushirikiana na Mkuu wa Majeshi pamoja na Waziri wa Ulinzi, kuzifanyia kazi changamoto zinazolikabili jeshi, ikiwa ni pamoja na maslahi ya wanajeshi.

### AWATAKIA KHERI KIDATO CHA 4

Katika hatua nyingine, Samia amesema serikali inaendelea kutengeneza mazingira mazuri na bora kwa wanafunzi nchini ili kuwawezesha waweze kutimiza malengo yao.

Aliyasema hayo jana kupitia ukurasa wake wa Instagramu alipokuwa akiwatakia mtihani mwema wanafunzi wa kidato cha nne ambao walianza rasmi kufanya mitihani hiyo ya taifa jana.

"Nawatakia kila la kheri wanafunzi wote wa kidato cha nne wanaoanza mitihani yao leo (jana)' na tunaendelea kujenga nafasi zaidi kwao ili kuwawezesha kusonga mbele kielimu, kiujuzi na kiajira," alisema Rais Samia.

Aliongeza kuwa serikali pia itaongeza nafasi za kidato cha tano na sita, vyuo vya ufundi stadi na mazingira bora ya nafasi zaidi za ajira ili kuwatengenezea mazingira wezeshi ya kutimiza ndoto zao.

# Watuhumiwa wa ujambazi wakamatwa, mmoja auawa D'Salaam

**Na Elizabeth Zaya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia watuhumiwa wanane katika matukio tofauti yakiwamo unyang`anyi wa kutumia nguvu, wizi wa magari.

Kadhalika, limedhibiti jaribio la wizi wa gari moja pamoja na kukamata gari moja lililokuwa limeibwa.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Muliro Jumanne Muliro, alisema watuhumiwa sita kati ya hao wamekuwa wakitumia mbinu ya kuwafunga walinzi kamba pamoja na plasta kabla ya kutenda uhalifu.

Alisema watuhumiwa hao sita waliokuwa wakitumia kamba na plasta kabla ya kufanya uhalifu walikutwa na Dola za Kimarekani Dola 2,000, kompyuta mpakato, saa za mkononi aina mbalimbali, simu nne na gari moja aina ya GAIA lenye namba za usajili T.274 CBH, vilivyoporwa maeneo ya Upanga.

Muliro alisema pia lilifanikiwa kupambana na majambazi wanne waliotaka kuiba gari katika eneo la Kibamba, Ubungo na mmoja kati ya hao alifariki wakati akikimbizwa hospitali kwa matibabu.

Alisema tukio hilo lilitokea juzi saa tatu asubuhi baada ya majambazi hao wanaokadiriwa kuwa wanne wakiwa na silaha, wakitumia gari aina ya Toyota Carina lenye namba za usajili T.374 DKR rangi ya dhahabu.

Alisema kabla ya hawajatimiza azma yao hiyo ya uporaji, kikosi kazi cha kuzuia na kupambana na uhalifu sugu kilifika eneo la tukio.

"Na majambazi hao walipobaini kuwa ni askari walianza kuwarushia risasi na Polisi wakajihami na kufanikiwa kumjeruhi mmoja ambaye alikimbizwa hospitali na baadaye alipoteza maisha. Juhudi za kuwatafuta majambazi waliokimbia zinaendelea, "alisema Muliro.

Katika tukio jingine, Mulilo alisema jeshi hilo lilifanikiwa kuzuia jaribio la uporaji wa gari Kibamba Wilaya ya Ubungo. Pia, walikamata gari namba T.775M DUM Toyota RACTIS lililokuwa limeibiwa na kutolewa taarifa katika kituo cha Polisi Kigamboni.

# Sabaya ashindwa tena kufika kortini

**Na Allan Isack,**
ARUSHA

WASHTAKIWA katika kesi ya uhujumu uchumi namba 27 inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya na wenzake sita, wamekwamisha kuendelea kusikilizwa kwa shauri hilo baada ya kushindwa tena kufika mahakamani jana.

Ole Sabaya na wenzake wanakabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha. Katika shauri hilo, mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine ni Silvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31) wanakabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu uchumi.

Akizungumza mahakamani huko, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Othmed Mtenga, alidai kwamba kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa mfululizo, lakini washtakiwa wote hawakufika mahakamani.

Mtenga aliiomba mahakama hiyo kuahirisha shauri hilo hadi washtakiwa hao watakapofika mahakamani huko kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa shauri hilo.

Wakili wa Utetezi, Mosses Mahuna, alidai hawana pingamizi la kuahirishwa kwa kesi kwa kuwa washtakiwa wote hawakufika mahakamani.

Baada ya kusikiliza ombi la Wakili wa Jamhuri, Hakimu wa Mahakama hiyo, Patricia Kisinda, aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 16, mwaka huu, majira ya saa 3:30 asubuhi itakapotajwa tena.

Katika shtaka la kwanza, washtakiwa wanadaiwa kuongoza genge la uhalifu kinyume cha Sheria ya Uhujumu Uchumi kifungu cha 57(1) na 60(2) na linawakabili washtakiwa wote.

Ilidaiwa mahakamani huko kwamba kwa pamoja washtakiwa hao Januari 22, mwaka huu, katika maeneo tofauti ya Jiji la Arusha, walifanya vitendo vya uhalifu kwa kujipatia fedha kiasi cha Sh. milioni 90 kwa manufaa yao.

Katika shtaka la pili ni la kujihusisha na vitendo vya rushwa linalomkabili mshtakiwa wa kwanza peke yake, indaiwa kwamba Januari 22, mwaka huu, eneo la Kwa Murombo jijini Arusha, Ole Sabaya alijihusisha na vitendo vya rushwa kwa kumtaka Francis Mroso kumpatia Sh. milioni 90 kwa kumshinikiza ili asitoe taarifa za jinai za madai ya ukwepaji kodi. Kwenye shtaka la tatu la kujihusisha na vitendo vya rushwa linalomkabili mshakiwa wa kwanza peke yake, inadaiwa kuwa Januari 22, mwaka huu, Ole Sabaya akiwa katika eneo la Kwa Morombo jijini Arusha, alijihusisha na vitendo vya rushwa kwa kujipatia Sh. milioni 90 kutoka kwa Francis Mroso ili asitoe taarifa za jinai za mtu huyo za madai ya ukwepaji kodi.

Shtaka la nne ni la matumizi mabaya ya madaraka linalomkabili Sabaya peke yake, ikidaiwa kuwa Januari 22, mwaka huu, akiwa katika eneo la Kwa Murombo jijini Arusha, alitumia vibaya nafasi yake ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, kumtisha Francis Mroso kumfungulia mashtaka ya kukwepa kodi.

Shtaka la tano ni la utakatishaji wa fedha na linawakabili washtakiwa wote saba, ikidaiwa kuwa Februari 22, mwaka huu, Ole Sabaya kwa kushirikiana na wenzake, wakiwa katika eneo la Kwa Murombo, walijipatia Sh. milioni 90, wakitambua kwamba kufanya hivyo ilikuwa ni zao la vitendo vya rushwa.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

## TANGAZO KWA UMMA

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, ipo katika hatua ya maandalizi ya mradi wa Uendelezaji wa Bonde la Mto Msimbazi (Msimbazi Basin Development Project) kwa kutumia fedha za mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Dunia. Mradi huu utatekelezwa na Wakala wa Barabara za Mijiji na Vijijini (TARURA) kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Halmashauri ya Manispaa za Kinondoni, Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo na Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe na Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS) kwa niaba ya Wizara husika zilizotajwa hapo juu.

**Mradi unatarajiwa kutekeleza masuala yafuatayo.**

1. Kukabiliana na kujikinga na mafuriko; Mradi unatarajiwa kujenga miundombinu ambayo itakuwa na uwezo mkubwa wa kupeleka maji baharini bila kutuama au kufurika katika maeneo ya bondeni. Miundombinu hiyo itajumuisha kuimarisha kingo za mto katika maeneo korofi ili kudhibiti mmomoyoka wa udongo kwa maeneo ya kati na mwanzo wa mto Msimbazi; kujenga makinga mchanga (sand traps) katika maeneo ya kimkakati; kujenga vituo/karakana za kutunza mto; kuhamisha wahanga wa mafuriko katika maeneo ya mabondeni; kuchimba na kupanua mto kuanzia barabara ya Kawawa hadi Daraja la Selander; na kujenga matuta yenye vimo tofauti kwa ajili ya kuruhusu maji kupita kwa usalama katika kipindi cha mafuriko; kuruhusu matumizi mbalimbali ya ardhi ikiwemo city park na uendelezaji wa maeneo ya makazi na biashara.

2. Ujenzi wa Miundombinu Stamihilivu ya Usafiri; Mradi unatarajiwa kujenga daraja jipya la Jangwani ambalo litakuwa na kimo kirefu ambacho hakitaathiriwa na mafuriko. Vilevile mradi utaboresha miundombinu ya usafiri (yaani barabara na madaraja) yaliyoungana na Bonde la Mto Msimbazi ambayo yanaathiriwa na mafuriko.

3. Udhibiti wa Mmomonyoko wa Udongo na Usimamizi wa Taka Ngumu; Mradi unatarajiwa kufanya kazi mbalimbali ambazo zitazuia mmomonyoko wa udongo na kudhibiti taka ngumu ili maji ya mvua yaweze kupita bila kizuizi kuelekea baharini. Kazi hizo zitahusisha upandaji miti katika misitu ya Pugu na kingo za mto, utunzaji wa mikoko na maeneo oevu, kuendesha programu ya usimamizi wa taka ngumu katika Kata zote zilizopo katika bonde la mto Msimbazi.

4. Usimamizi wa Mipango Miji katika "Msimbazi Special Planning Area"; Matuta yatakayojengwa na mradi yatapelekea kuwepo na maeneo salama kwa ajili ya "City Park" na uendelezaji wa mji (makazi na biashara) pembezoni mwa bonde la mto Msimbazi kama ilivyopendekezwa katika Mpango wa Fursa wa Msimbazi (Msimbazi Opportunity Plan). Mradi utasaidia kuandaa mpango wa kina wa matumizi ya ardhi (Detailed Land Use Plan) ambao utakuwa shirikishi kwa wadau wote. Vilevile mradi utazijengea uwezo mamlaka husika ili ziweze kusimamia utunzaji wa "City Park" na uendelezaji wa mji kadiri ya matumizi ya ardhi yaliyopangwa.

Lengo la tangazo hili ni kuujulisha umma na wadau wa Bonde la Mto Msimbazi kuwa timu za wataalam kutoka Taasisi husika pamoja na Wataalam Washauri zinazofanya upembuzi yakinifu na usanifu zitapita katika baadhi ya maeneo ili kufanya mashauriano na wadau kwa njia mbalimbali ikiwemo mikutano, mahojiano na dodoso. Tarehe, muda na mahali pa kufanya mashauriano zitatolewa kwa wakati muafaka. Aidha, tahadhari zote kuhusiana na UVIKO -19 zitachukuliwa katika kipindi hiko.

**KATIBU MKUU**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kwa:**
**Baruapepe: cities.project@tamisemi.go.tz; cities.project@yahoo.com**
**Simu: +255 22 270 0769**

2165602



Mkurugenzi wa Kampuni ya KCG Aquatec Fish Farming Consultancy, Stephano Karoza, akitoa elimu ya ufugaji wa samaki kwenye vizimba katika Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# KESI YA MBOWE
# Mawakili utetezi wakomaa shahidi aliyeingia na 'diary'

**Na Kula Mzee**

MAWAKILI wa utetezi, Jeremiah Mtobesya na Peter Kibatala, wameomba mahakama imwondoe shahidi wa Jamhuri aliyekutwa na diary (kitabu cha kumbukumbu za kila siku) kizimbani, Koplo Msemwa asiendelee kutoa ushahidi na ushahidi alioutoa Ijumaa iliyopita uondolewe kwenye kumbukumbu za mahakama kwa madai kuwa hafai na hakidhi vigezo.

Hoja hizo ziliwasilishwa jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga, wakati kesi hiyo ya ugaidi inayomkabili, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe na wenzake watatu ilipokuwa ikiendelea kusikilizwa kesi ndogo.

Kabla ya hoja ya diary, Mahakama hiyo ilipokea kielelezo cha barua kutoka kwa Msajili kwenda kwa Koplo Msemwa iliyokuwa ikimwezesha shahidi kupata kielelezo cha kitabu cha kumbukumbu za watuhumiwa Kituo cha Polisi cha Kati Dar es Salaam.

Baada ya kupokelewa kwa barua hiyo iliyokuwa ikipingwa na upande wa utetezi, Jaji Tiganga alimruhusu shahidi kuisoma, lakini Wakili Mtobesya alipinga kwa madai kwamba kulikuwa na uamuzi kuhusu diary ni muhimu unapaswa kutolewa.

Mtobesya alidai Novemba 12, mwaka huu, shahidi akiwa kizimbani anatoa ushahidi kwenye kesi ndogo, alionwa akiwa na diary, simu na kalamu.

Alidai wakati Wakili Peter Kibatala anatoa hoja, diary hiyo ilikuwa wazi na baada ya kuwasilisha hoja Mahakama iliona busara kumrejeshea simu na kubakia na diary.

"Leo sisi tuko tayari kuelezea ni kwanini shahidi huyu asiendelee kutoa ushahidi wake na kisha Kibatala atamalizia kuwasilisha hoja zake pia," alidai Mtobesya.

Alidai suala hilo limejitokeza katikati ya mwenendo wa shauri, shahidi aliyekuwa kizimbani anaruhusiwa kuwa na nyaraka yoyote endapo ataruhusiwa na mahakama na ruhusa itatoka pale anapotakiwa kufanya rejea.

Mtobesya alidai ikitokea kuna umuhimu wa kiambatanisho au nyaraka kuingia mahakamani basi utaratibu utafuatwa na uliotajwa kwenye sheria ya mwaka 2019 sura ya 200 ni shahidi kuomba ruhusa kwa mahakama.

"Hizi taratibu lazima zifuatwe ili washtakiwa wapate haki zao wakati wa maswali ya dodoso, ikitokea shahidi kafanya kwa kificho inamnyima haki mshtakiwa ya kujua shahidi alirejea kwenye nini.

"Kwa kuwa hakuomba ni hisia zetu kuwa aliingia na diary, kwa mawasilisho haya mheshimiwa jaji shahidi huyu asiendelee kutoa ushahidi wake na ushahidi aliotoa uondolewe kwenye kumbukumbu za Mahakama.

"Mahakama yenye uwezo wa kumwondoa shahidi ni Mahakama hii, ni msimamo wetu kuwa shahidi alikuwa akitoa majibu kwenye diary wakati anatoa ushahidi.

"Na kwa sababu amefanya hivyo kabla hajamaliza kutoa ushahidi wake basi tunasema hafai," alidai Mtobesya.

Akiwasilisha hoja Wakili Peter Kibatala alidai ni misingi ya kisheria kwamba hairuhusiwi kuwa na nyaraka kizimbani isipokuwa kifaa kazi cha uapishaji.

"Kwa mujibu wa sheria, ahahidi ambaye ameingia na nyaraka isiyoruhusiwa sio shahidi sahihi, kwanza kwa kuingia nayo na pili kwa kushindwa kuomba ruhusa.

"Wenzetu watakuja na hoja shahidi anaruhusiwa kuwa na kidaftari kidogo, katika muongozo wa Polisi kuna masharti yake kidaftari hicho kinatakiwa kuandikwa kwa penseli.

"Kama kumwondoa shahidi ni hatua kali basi turuhusu tuone alikuwa anaandika nini humo, majina ya askari aliokuwa anawataja, tarehe alizokuwa anataja au taarifa aliyokuwa anatoa," alidai Kibatala.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Abdallah Chavula, akijibu hoja za utetezi, alidai msimamo wao hawakubaliani na misingi ya hoja za upande wa utetezi, lakini hawakubaliani na maombi yaliyowasilishwa.

Alidai mwongozo wa Polisi (PGO) unatoa maelekezo kwamba ofisa wa polisi anapokuwa anatoa maelezo lazima awe na daftari na sharti la pili kabla hajaenda mahakakamani afanye marejeo.

"Kwa mujibu wa PGO kifungu B kinasema kwa ruhusa ya jaji au hakimu mmiliki anaweza kurejea kumbukumbu pekee na siyo kwa dhumuni la kusoma au kuelezea kilichoandikwa.

"Pangekuwa na katazo pangewekwa wazi kwamba ni marufuku, wakati hayo yanatokea shahidi alikuwa hatoi ushahidi, alikuwa akisikiliza malumbano.

"Wakati shahidi anaongozwa kuanzia maapisho mpaka anatoa ushahidi wake, Mahakama ilikuwa ikimtazama, hakuna hata mmoja wetu aliyesimama kwamba shahidi alikuwa akiongozwa na kuna vitu alikuwa anasoma, kuvirejea, hiyo hoja haikuletwa," alidai Chavula.

Alidai hakuna mahali ilionyesha kuwa shahidi haelewi na majibu aliyokuwa anatoa hayana mahusiano mbele ya mahakama na pili hakuna mahali ilipoelezwa kuwa wakati anahojiwa na mwendesha mashtaka alishindwa kujibu maswali.

"Sababu ya kumwondoa shahidi ni umri mdogo, hakuna nguvu ya kisheria ya kufanya mahakama yako iondoshe shahidi na iondoshe ushahidi wake," alidai Chavula.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Pius Hillar, akiongezea alidai hoja za mawakili wa utetezi hazipo sawasawa na Mahakama haijaelekezwa kwa kujitosheleza.

Alidai shahidi alikuwa anatoa majibu kutokana na uelewa wake, pande zote zilikuwapo wakati akimwongoza kutoa ushahidi.

"Mimi nilikuwa karibu na shahidi kuliko mtu mwingine, Mheshimiwa Jaji hukuona shahidi akisoma wakati anatoa ushahidi wake, haya ni masuala ya kisheria yanapaswa kwenda kisheria," alidai Hillar.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Adamu Kasekwa, Mohammed Ling'wenya na Halfani Bwire, washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka sita ikiwamo kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kumdhuru aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

Matukio hayo yalitarajiwa kufanyika Dar es Salaam, Arusha, Morogoro, Moshi, Mwanza na Mbeya.

**JAJI KUTOA UAMUZI LEO**

Baada ya upande wa Jamhuri kumaliza kujibu hoja za mawakili wa utetezi, mahakama ilitoa nafasi kwa mawakili wa utetezi kumalizia kujibu kama wana hoja za nyongeza.

Wakili Mtobesya alidai shahidi na upande wa mashtaka hawakufanya matakwa ya kisheria ili shahidi awe na nyaraka ambayo amekutwa nayo kizimbani.

"Mahakama imchukulie shahidi huyo sio mkweli, hajiwezi na haaminiki kamwe, mheshimiwa jaji mahakama ione ombi letu lina mashiko na itupatie nafuu kama ambayo tuliwasilisha mwanzoni," alidai Mtobesya.

Wakili Kibatala aliomba jaji aangalie katika hoja za upande wa Jamhuri, hakuna wakili hata mmoja aliyegusa hoja ya kifungu cha 62 cha Sheria ya Ushahidi kuhusu sifa za shahidi.

"Mawakili hawajajibu kabisa katika diary shahidi alikuwa anaweka mambo yake binafsi kama masuala ya MANYU na ASNO, ushahidi unaanza pale tu shahidi alipoapishwa.

"Hoja kwamba hivyo vifungu havitoi zuio kwanini walisema kwa ruhusa ya Mahakama, kwanini walisema upate kibali, anayesema hakuna katazo haungwi mkono na sheria," alidai Kibatala na kumaliza hoja za upande wa utetezi.

Jaji Tiganga alisema pande zote mbili walifikia mwisho wa kuwasilisha hoja zao, Mahakama inaratajiwa kutoa uamuzi.

"Tumefikia mwisho kama mlivyoona, mmetumia siku nzima inamaana na mimi nitumie siku nzima kuandika uamuzi kwa namna ambavyo hoja zimewasilishwa," alisema Jaji Tiganga.

Jaji aliahirisha shauri hilo hadi leo saa tano asubuhi kwa ajili ya kutoa uamuzi.

## Riba kubwa mikopo chanzo urejeshaji kukwama

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema riba kubwa kwenye mikopo, ni kati ya sababu za wakopaji kushindwa kurejesha mkopo huku wengine kutoroka na kusababisha uchumi kudorora.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba, alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki, akifunga Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa, iliyofanyika viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam.

Tutuba, alibainisha kwamba wakati akitembelea mabanda ya taasisi za kifedha za umma na binafsi, ameshuhudia watoa huduma za mikopo kwa wananchi kuwa na riba ya asilimia 25.

"Watoa huduma za kifedha wana riba kubwa ambayo inakaribia kulingana na faida yao ambayo ni asilimia 10 hadi 25, inawezekana inamfanya mfanyabiashara ashindwe kurejesha mkopo na kutokomea.

"Mkopaji pia lazima ajulikane, tutafungua dirisha la usajili la wakopaji ili wafahamike, namna ya kuwapa na kuzijua historia zao katika ukopaji na urejeshaji," alisema Tutuba.

Pia alieleza kwamba hivi sasa hati fungani za mtaji mdogo zinapatikana ili kufanikisha walio na mitaji midogo kuwekeza shughuli zao.

Julai, mwaka huu, Gavana wa Benki Kuu (BoT), Prof. Flourens Luoga, alisema benki hiyo imetoa mwongozo wa benki za biashara kupunguza riba kwa sekta binafsi.

Alisema BoT, imetenga fungu la Shilingi trilioni moja zitakazotumika kuzikopesha benki na taasisi za fedha kwa riba ya asilimia tatu na benki zitoe mikopo kwa riba isiyozidi asilimia 10.

Awali, kabla ya kufunga Wiki ya Huduma za Fedha Kitaifa, viwanjani hapo, Kamishna wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango. Dk Charles Mwamwaja, alisema jumla ya mabanda 100 yalishiriki na kutoa elimu ya kifedha.

Alisema elimu iliyotolewa ni kuhusu, usimamizi wa fedha, mikopo, akiba, hati fungani na kutambua thamani ya sarafu na utunzaji wake na utatuzi wa malalamiko yaliyopo katika sekta hiyo.

HABARI KITAIFA

# Majaliwa achukizwa kiwanda kuziba reli

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekerwa na kitendo cha Kampuni ya Kiluwa inayozalisha nondo kuziba reli iliyojengwa na serikali kwa ajili ya kurahisisha usafiri wa bidhaa zinazozalishwa katika kiwanda hicho.

Majaliwa amefanya ziara ya siku moja katika kiwanda hicho kilichopo Mlandizi, Kibaha jana kukagua uzalishaji na pia alilenga kuangalia reli iliyounganishwa na serikali miaka mitatu iliyopita.

Akiwa katika kiwanda hicho Majaliwa alikagua reli hiyo ambayo alishuhudia ikiwa imezibwa na zege na maeneo mengine ikiwa imejaa mchanga na haitumiki kama kampuni hiyo ilivyoomba awali.

"Hii imeunganishwa kutoka reli ya kati kuja hapa kwa gharama ya serikali na inatokana na maombi ya kampuni yenu kinachoshangaza hali hii kuona mmeweka ukuta eneo la reli kuigia ndani na sehemu nyingine mmeweka kabisa zege," alisema.

Vile vile, alisema serikali italeta tume kuchunguza yaliyofanyika kuhusu reli hiyo na kwamba anatambua kuna mambo mengi yatagundulika ikiwamo la kutokuwa na maelewano na Mtanzania aliyewaunganisha hapo.

"Mara ya mwisho kuingia katika kiwanda hiki ni mwaka 2017 na leo nimekuja kukagua uzalishaji na reli iliyojengwa kama kweli inafanya kazi kama ilivyoombwa na Mtanzania ambaye ni Mohamed Kiluwa mwekezaji mwenye shea kwenye kampuni hii," alisema Waziri Mkuu.

Alisema serikali inaendelea kuhamasisha uwekezaji na wanaopata nafasi wanatakiwa kuheshimu sheria za nchi kama ilivyo kwa Watanzania wanavyofanya wakiwa China. Aliwataka wawekezaji wa kiwanda hicho walioanza migongano na Mtanzania huyo kuepusha kugombanisha Tanzania na China na badala yake kusimamia sheria na taratibu zilizopo.

Alisema ameshangazwa na kitendo cha Kampuni ya Kiluwa ambao sasa wanamgongano hadi kufikishana mahakamani kutokana na kukiukwa kwa baadhi ya makubaliano hususani upande wa hisa jambo ambalo linahatarisha kuondoa mahusiano mazuri yaliyopo kati ya nchi hizo mbili.

"Hiki ninachokiona hapa nimekishuhudia Mafinga mnataka kumwondoa Mtanzania kwenye shea zenu hata jina lake kulifuta mpaka mnapelekana mahakamani hii haileti picha nzuri, serikali yetu ina mahusiano mazuri na China sasa tusifikie kuyaharibu tufuate sheria," alisisitiza.

Aliwataka wanasheria wa kampuni hiyo kutolinda uovu wa wawekezaji badala yake kusimamia sheria na taratibu zilizopo.

Alisema atamwagiza Waziri wa Ajira kufika katika kiwanda hicho na kuongea na wafanyakazi kusikiliza kero zao ili zipatiwe ufumbuzi wa haraka.

Mmoja wa wafanyakazi wa Kiluwa alisema wanakabiliwa na kero ya mishahara kuwa midogo na kukosa vifaa vya kazi, na sare walizovaa wamepewa siku ya ziara ya Waziri Mkuu.

Kwa upande wake Kiluwa alisema kuwa bado yumo ni kati ya wakurugenzi wa kampuni hiyo ingawa hajaingia katika kiwanda hicho kwa miaka mitatu.

Alisema ametofautiana na wakurugenzi wengine ambao ni raia wa China kutokana na kuvunja taratibu walizokubaliana pamoja na matumizi ya fedha yasiyoeleweka. Alisema tangu kiwanda hicho kizinduliwe hajawahi kupata mshahara na sasa wamefikisha kesi mahakamani ya kudai kupata hisa zake ambazo anazozuiwa kuzipata kwa muda mrefu huku akizuiwa pia kuingia ndani ya kiwanda hicho.

Mwakilishi wa upande wa Wachina wanaoendesha kiwanda hicho, Want Shengju, alisema reli ya kuingia katika kiwanda hicho imefukiwa na mchanga kwa muda mrefu na watasafisha kuonyesha njia zilizopita reli.

## Mwakilishi wa PM Uingereza kuja

**Na Salome Kitomari**

MWAKILISHI wa biashara wa Waziri Mkuu wa Uingereza, Walney John Woodcock, anawasilia leo nchini kwa ajili ya uzinduzi wa Jukwaa la Biashara la kwanza kati ya nchi hiyo na Tanzania.

Kiongozi huyo na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kesho watafungua jukwaa hilo litakalowajumuisha watumishi wa serikali na wafanyabiashara kujadili fursa na kuongeza uwekezaji na biashara kati ya nchi hizo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na Ubalozi wa Uingereza nchini, zaidi ya wafanyabishara 125 watashiriki jukwaa hilo moja kwa moja na wengine kwa njia ya mtandao kujadili masuala ya biashara na uwekezaji kwa nchi hizo.

Aidha, watajadili changamoto na fursa zilizopo kulingana na sekta, mambo ambayo yatasaidia kuboresha mazingira ya biashara na kuwa na sekta binafsi imara inayotoa ajira na kuchangia ukuaji wa uchumi.

"Hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa mwakilishi wa ujumbe wa biashara kwa Tanzania. Pia atakutana na Rais Samia Suluhu Hassan," ilisema taarifa hiyo.

Pia, ujumbe huo utakuwa na kikao maalum na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Liberata Mulamula; Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. KItila Mkumbo na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe.

Aidha, atakutana na wafanyabiashara na wawakezaji Dar es Salaam na Arusha, ikiwa ni namna ya kuimarisha uhusiano wa kibiashara wa Uingereza kwa Tanzania.

Akizungumzia safari yake hiyo, alisema: "Nina furaha kutembelea Tanzania, nitazindua jukwaa la biashara ikiwa ni alama ya kuanza kwa majadiliano yatakayojenga maelewano na mtazamo mmoja kwa nchi zetu. Wafanyabiashara wa Uingereza ni miongoni mwa wawekezaji Tanzania. Ni matamanio yangu kuona wanaongezeka siku zijazo."



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akiwasha mshumaa, kuashiria kupokea mwaka mpya wa Kihindu, kwenye sikukuu ya Diwali na sherehe za mwaka mpya wa Kihindu, zilizofanyika, Kisutu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# TCC ilivyotoa ajira kwa maelfu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Sigara Tanzania (TCC), imesema moja ya mafanikio yake ya miaka 60 ya kuanzishwa kwake ni kutoa ajira kwa maelfu ya Watanzania.

Kampuni hiyo ilizinduliwa na Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere Desemba 4, 1961, siku chache tu kabla ya Tanzania kutangazwa kuwa taifa huru na Uingereza.

Hayo yalibainishwa jana mkoani Dar es Salaam na Patricia Mhondo, Mkurugenzi Uhusiano na Mawasiliano wa TCC wakati wa ziara ya wahariri wa vyombo vya habari katika kiwanda cha kuzalisha sigara.

Patricia alisema kwa sasa TCC imetoa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa Watanzania 2,749 kati ya ajira takribani 40,000 zinazotolewa na kampuni mama ya JTI duniani.

Mbali na utoaji wa ajira za maelfu kwa Watanzania, alisema TCC imeendelea kujipanua na kutoa mchango mkubwa kwa serikali, ikiwamo kodi.

Alisema: "Tunapoendelea kujitanua, mchango wetu kwa serikali pia umeongezeka na kufikia wastani wa kodi ya zaidi ya shilingi bilioni 200 kwa mwaka. Kwa mujibu wa Patricia, mchango na utendaji wa TCC kwa ujumla umekua mara kwa mara kwa miaka mingi na kufikia uwezo wa uzalishaji wa vijiti vya sigara bilioni 10 kwa mwaka, huku ikidumisha wastani wa hisa asilimia 90 ya soko katika kipindi cha miezi 18 iliyopita.

Kwa upande wake, Michael Bachan, Mkurugenzi Mkuu wa TCC (Plc) alisema: "Mwaka huu, TCC (Plc) inaadhimisha miaka 60 ya kazi kwa mtindo huku tukiendelea kurekodi matokeo bora. Licha ya changamoto za Uviko-19 katika kipindi cha miaka 2 iliyopita, TCC (Plc) imerekodi utendaji bora katika nusu ya kwanza ya mwaka.

Alisema kiasi cha mauzo ya ndani na nje kimeongezeka kwa asilimia 16.5 na asilimia 3.7 kwa mtiririko huo huku kiasi cha jumla kikiongezeka kwa asilimia 12.5.

Bachan, alisema ukuaji huu wa kiasi unaonyesha nguvu ya muundo wa usambazaji wa ndani uliorekebishwa. "Kwa matokeo haya, kampuni ina matumaini kuhusu matokeo ya nusu ya pili ya mwaka."

Alisema wanaamini kuwa hilo limewezekana kwa sababu ya kujitolea bila kuyumba kwa wafanyakazi wao, ambao ni mali kwa shirika na mchango muhimu kwa biashara.

Bachan aliongeza: "TCC (Plc) inazingatia kuwekeza katika afya ya watu, ustawi na vipaji na kwamba imeboresha mienendo ya kufanya kazi na kuinua viwango ambavyo vimekubalika kitaifa na kimataifa.

Alisema mwaka 2021, kampuni ilitambuliwa kama 'Mwajiri Bora' kwa mwaka wa nne mfululizo na Taasisi ya Mwajiri Bora.

Aidha, alisema ilipata cheti cha kiwango cha dhahabu katika cheti cha 'Wawekezaji katika Watu', tathmini ya jinsi kampuni inavyotoa utamaduni uliooreshwa wa kufanya kazi kwa kuwaweka watu wao mbele na kuweka uwiano sahihi wa maisha ya kazi kwa ajili ya kujenga afya bora na yenye nguvu zaidi, jamii yenye furaha zaidi.

Aliongeza kuwa kwa miaka mingi, uongozi imara na uwekezaji thabiti kwa watu umefungua njia kwa Watanzania 25 kufanya kazi za kimataifa katika nyadhifa mbalimbali nje ya Tanzania (mfano kama Makamu wa Rais, Wakurugenzi na Mameneja) katika nchi mbalimbali zikiwamo Uswisi, Uingereza, Canada, Nigeria, Zambia, Malawi, Sudan, Geneva, Iran, Jordan, Ethiopia na Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE). Kadhalika, alisema TCC inaendelea kutoa kwa jamii moja kwa moja na kwa njia nyingine kupitia ushirikiano na washirika wa kijamii na kitamaduni

kukuza mageuzi kamili na endelevu ya maisha.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Stendi Tegeta sasa iwekewe huduma

**MOJA** ya kilio kikubwa cha watumiaji wa kituo cha daladala cha Nyuki, Tegeta Wilaya ya Kinondoni Dar es Salaam, ni ubovu wa kituo hicho ambacho hakina huduma muhimu za kijamii kama choo, hali inayowafanya watumiaji kupata shida.

Licha ya hali hiyo, watumiaji hao hususan madereva na makondakta wanatakiwa kulipa ushuru wa Sh. 1,000 kwa kila gari linaloingia kushusha na kupandisha abiria na kwa namna eneo lilivyo hakina hadhi ya kuitwa kituo ambacho serikali inakusanya mapato.

Magari yanayoingia na kutoka kituoni hapo ni yanayofanya safari za Bunju, Posta, Kivukoni, Kariakoo, Morocco, Mawasiliano, Bagamoyo, Mbezi, Madale na Msata. Hali ya geti na barabara ya kuingia kituoni humo ni kero kwa wenye magari, watembea kwa miguu na wenye maduka ya biashara.

Magari yote yanatoka na kuingilia kwenye geti moja, hali inayosababisha msongamano, hakuna taa, uchafu umetapakaa, hakuna maeneo ya abiria kupumzikia na hivyo mvua na jua kuwa vyao. Mbaya zaidi, wakati wa mvua kuna tope jingi na usumbufu mkubwa.

Choo kinatotumiwa ni cha soko na kinamilikiwa na mtu binafsi, jambo ambalo ni usumbufu mkubwa kwa eneo ambalo manispaa inakusanya fedha kila siku, lakini hazirudi kufanya maboresho kwenye chanzo hicho ili kuongeza mapato zaidi.

Watumiaji wa kituo hicho ni mama lishe, wafanyabiashara ndogo, madereva, wasafiri na wanaopokea wasafiri, lakini mazingira magumu yaliyopo humo yanawafanya wengi kutotumia na kuyasubiri magari nje au barabarani.

Manispaa ilipoulizwa na Nipashe, ilisema zabuni ya ujenzi wa kituo hicho na cha Bunju zimeshatangazwa na matangazo yamebandikwa sehemu mbalimbali, ingawa kwa sasa nguvu kubwa imeelekezwa kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Tunaona pamoja na shughuli nyingi za manispaa, lakini lazima vituo vya daladala ambavyo ni chanzo cha mapato vikatazwamwa kwa jicho la tofauti ikiwamo kuhakikisha vinakuwa na huduma zote muhimu.

Moja ya vyanzo vya mapato vya serikali za mitaa ni pamoja na vituo vya daladala na mabasi, na haiwezekani iwe ni sehemu ya kukusanya fedha tu bila kurudisha kwa kufanya maboresho muhimu ili kiingize fedha zaidi.

Bado kuna nafasi ya kujenga choo cha kisasa kwa ushirikiano na sekta binafsi, kuliko kusubiri upatikanaji wa fedha ndipo ujenzi uanze, huku watumiaji wakiumia, lakini hakina hadhi ya eneo husika.

Kutokana na miundombinu duni hali ya usafi siyo ya kuridhisha jambo ambalo ni hatari kwa watumiaji wote, na afya zao kuwa hatarini. Ndiyo maana tunaona ni muhimu sana kituo hiki kikaboreshwa kwa kuwekewa miundombinu muhimu ili isiwe ni ng'ombe anayekamuliwa bila malisho licha ya afya yake mbaya.


Kituo hicho ni kimoja kati ya vingi ambavyo manispaa inakusanya fedha, lakini hazirudi kwa ajili ya kukihudumia, lakini bado kuna nafasi ya kuwekeza na fedha ikarudi ikiwa wataweka ofisi na vibanda vya biashara vitakavyowezesha watu kupangisha.

Ni muhimu sana ubunifu wa kuboresha vyanzo vya mapato ukawepo kwa kuwa kukiwa na vituo vizuri kunabadili mwonekano wa eneo husika, kuna kuza maendeleo lakini mapato yatapatikana kwa wingi na rahisi zaidi huku afya za watumiaji zikibaki salama.

Kwa sasa maboresho yamefanyika kwenye baadhi ya masoko lakini kuna maeneo hayajafanyika, kiasi cha miundombinu kuwa mibovu hasa nyakati za mvua na hatarishi kwa afya za watumiaji. Walipa kodi wanataka kuona miundombinu bora kwenye vituo na masoko au sehemu zote za huduma za kijamii, inapokuwa tofauti wanaona kuwa hawakustahili kupata huduma muhimu na itaathiri chanzo cha mapato.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Wajibu wa serikali, wamachinga sakata la biashara ndogo mijini

Na Askofu William Mwamalanga

**CHANZO** cha matajiri wakubwa na mabilionea duniani ni wafanyabiashara wadogo pengine wakianzia kazi zao mitaani kama wanavyofanya wamachinga.

Baadhi ya mabilionea ambao kazi zao zinaonekana duniani kote leo, walianza na umachinga na mmoja wao ni mmiliki wa mgahawa wa KFC.

KFC ni jiko linalopika chips na kuku lililoanzishwa na kanali Harland Sanders, mjasiriamali aliyeanza shughuli zake kwakuuza kuku waliokaangwa kwenye mgahawa wake uliokuwa pembeni ya barabara uliokuwa Corbin jijini Kentucky, nchini Marekani.

Sanders, alianzisha mgahawa huo tangu mwaka 1952 na sasa umesambaa dunia nzima na hata Dar es Salaam na mikoani, jiko la KFC linajulikana.

Ndiyo maana ni vyema serikali ikatambua kuwa biashara ndogo za wamachinga ni mwanzo wa ajira rasmi na tena ni mwanzo wa mabilionea wa miaka ya sasa na ijayo.

Biashara hizo ni ajira muhimu na ndicho chanzo cha kumaliza umaskini na kujenga uchumi imara , iwapo zitasimamiwa kikamilifu.

Kamati ya Kitaifa ya Maaskofu na Mashekhe ya Maadili, Amani na Haki za Binadamu kwa Jamii ya Madhehebu ya Dini, wakati wa mazungumzo na baadhi ya vijana wasomi jijini Dodoma, inashauri serikali kuzitambua biashara hizo ndogo kuwa ni ajira rasmi na njia muhimu ya watu kujipatia kipato.

Maaskofu na Mashekhe wanakiri kuwa hapo awali waliwahi kumpelekea ushauri John Magufuli wakati huo akiwa rais na kumshauri jinsi ya kulinda na kuendeleza biashara hizo.

Maaskofu na Mashekhe wanaeleza kuwa walishauri kuwapo na kutoa uhuru wa machinga kufanya kazi bila bugudhiwa na serikali na kuzitambua rasmi biashara hizo kwani zina mchango mkubwa wa maendeleo ya nchi. Viongozi wa dini wanasema serikali ilianza na kuwatambua wamachinga ilipotoa vitambulisho ikiwa ni hatua ya kwanza.

Mpango huo unaweza kumaliza tatizo la ajira kwa vijana kwani tayari ndiyo taasisi kubwa inayoajiri watu wapya kila siku.

Wanaoingia kwenye ajira hizo si lazima wawe wasomi, hata wasiosoma hata darasa moja wapo. Kinamama, wazee, vijana na hata wenye mahitaji maalumu wana nafasi kwenye eneo hilo. Lakini kama serikali isiposikiliza ushauri wa wadau wakiwamo viongozi wa dini na wakiendelea hivi wanavyoilitatua tatizo hilo linaweza kuwa tatizo kubwa zaidi.

Viongozi wa dini wanaona wamachinga wote Bara na Visiwani mikoa yote washughulikiwe. Ndiyo maana wanashauri serikali baadala ya kuwatafutia wamachinga wa Dar es Salaam, eneo la Jangwani ili kuuza bidhaa zao, kazi iende mbele zaidi kwa mtazamo wa kuwasaidia popote walipo .

Kinachohimizwa sasa ni halmashauri za miji na majiji kutenga maeneo ya biashara kwa kushirikiana na wamachinga wenyewe.

Ni vyema kuwashirikisha wamachinga, kwenye kupata viwanja na maeneo ya kufanyia biashara, ili kuwapo na kuridhiana, ili kupunguza malalamiko.

Kwa wamachinga ni wajibu wao kufanyabiashara kama kazi ya kufanikisha maisha yao na siyo kubahatisha, mfano kuweka bidhaa popote hata juu ya makaro (chemba) za majitaka kutoka vyooni au reli si jambo jema.

Biashara hizo ni lazima zitumie teknolojia kwavile ndicho kitu kinachoendelea sasa. Aidha, ziende na wakati, vifungashio vya kulinda afya na zifanyike kutunza na kuhifadhi mazingira.

Hivyo wamachinga wanaposhirikiana na serikali za halmashauri kutambua na kuainisha maeneo ya biashara hilo walizingatie, mtumizi ya teknolojia siyo kufanya biashara kimazoea.

Katika uwekezaji huo wa kimachinga ni vyema pia kutambua mbinu na utaratibu wa kuboresha biashara ndogo ndogo na kuzibadilisha zisibakie vile vile miaka yote.

Kila mwaka ni kuuza bidhaa juu ya kiroba pembeni ya barabara, kadhalika kuuza pweza, kukaanga vyakula vingine karibu na mitaro ya majitaka, kutupa taka ovyo na kufanya biashara kwa mtindo mmoja kwamiongo yote.

# Mwanafunzi akutwa kajinyonga hadi kufa

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MWANAFUNZI wa Shule ya Msingi Lukobe, Egdilus Edmund (13), mkazi wa mtaa wa Tushikamane, Manispaa ya Morogoro, amekutwa amejinyonga hadi kufa chumbani kwa dada yake kwa kutumia kamba ya manila.

Chanzo cha kifo hicho hakijafahamika mpaka sasa.

Akielezea tukio hilo dada wa marehemu, Editha Edmund, ambaye alikuwa mtu wa kwanza kushuhudia tuko hilo, alisema siku ya tukio mdogo wake alikataa kwenda kanisani akidai anamalizia kazi za shule (homework), dada yake aliienda kanisani na baba yake aliienda kazini baadaye aliporejea nyumbani alimkuta mdogo wake ananing'inia juu ya paa akiwa tayari amefariki dunia.

Naye baba wa marehemu, Edmund Peter, alisema mwanawe hakuwa na tatizo la akili na alikuwa mtu mwenye furaha muda wote na kwamba tukio hilo linawapa maswali mengi kujua nini kilichomsibu kijana wao.

Mwenyekiti wa mtaa huo, Omary Hassan, alisema kuna haja ya wazazi kuwa karibu na watoto wao.

Alisema huenda sababu ni watoto kuishi na baba yao huku mama akiishi sehemu nyingine na mtoto huyo kushindwa sehemu ya kufikisha tatizo lililokuwa likimkabili.

Kamanda wa Polisi Mkoa Morogoro, Fortunatus Musilimu, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

# Wataka fidia kupisha mgodi

**Na Lilian Lugakingira,**BUKOBA

BAADHI ya wakazi wa Mkoa wa Kagera wamesema kuwa migogoro mingi katika maeneo ya uwekezaji imekuwa ikitokana na baadhi ya wawekezaji kutowashirikisha ipasavyo wanaokutwa katika eneo la mradi.

kuiomba serikali kusimamia wananchi wa Wilaya ya Ngara ambako utaanza mradi wa kuchimba madini aina ya nickel, ili kuhakikisha wanalipwa fidia zinazostahili.

Wakizungumza baada ya serikali kuitambulisha kampuni ya Tembo Nickel ambayo imepewa leseni kubwa na serikali Oktoba 27, mwaka huu kwa ajili ya kuanza mchakato wa kuchimba madini hayo katika Wilaya ya Ngara, mmoja wa wananchi hao, Pius Ngeze, walisema endapo watapewa haki yao wanayostahili hakutakuwa na mgogoro wowote.

"Sitarajii kuwapo mgogoro na hautatokea kama wananchi watatendewa haki, wanapaswa kutambuliwa kwamba wameishi katika eneo hilo kwa muda mrefu tangu enzi za mababu zao, hivyo lazima waondoke kwa utaratibu ambao hawatajuta kwa nini umekuwapo mgodi pale... kwa hiyo njia pekee ya kuzuia hilo lisitokee ni kuwashirikisha na serikali kusimamia haki zao," alisema Ngeze.

Naye Yegesa Mabara, alisema kuwa wananchi wa Kagera wanahitaji kupata maendeleo kiuchumi, hivyo sio rahisi kama wameshirikishwa ipasavyo wakashindwa kuhama kwa hiari, baada ya kulipwa haki zao kihalali.

"Sekta binafsi wanapofanya uwekezaji katika maeneo yanayokaliwa na wananchi bila kuwashirikisha ndicho chanzo kikubwa na kuzuka kwa migogoro, lakini kama ushirikishwaji umefanyika inavyotakiwa, nina imani wananchi wataitikia na kuupokea mradi huo bila tatizo, kwa ajili ya maendeleo endelevu ya mkoa na taifa kwa ujumla," alisema.

Akizungumza wakati wa kuipokea na kuitambulisha kampuni hiyo katika mkoa, Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Meja Jenerali Charles Mbuge, alisema utafiti katika eneo hilo umefanyika kwa muda mrefu wa takriban miaka 40 na kwamba hatua ya kampuni hiyo kupewa leseni kubwa kuanza kuchimba madini katika eneo hilo, imeleta matumaini kwa wakazi wa Kagera.

Alisema serikali iko pamoja na mwekezaji huyo, na kwamba haitaruhusu vikwazo kutoka kwa wananchi wasio waaminifu, ambao sasa baada ya kusikia mradi unakaribia kuanza, watakwenda katika eneo la mradi kujenga nyumba na kupanda mimea ya kudumu, ili wapate malipo na kuwa huo ni ukiukwaji wa sheria.

# Gondwe awapa siku 3 wamachinga waliovamia eneo la kanisa kuondoka

**Na Mary Geofrey**

SIKU moja baada ya Nipashe kuripoti 'Wamachinga' waliovamia na kufanyabiashara katika eneo la Kanisa la Orthodox, Jimbo la Dar es Salaam, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Godwin Gondwe, amewapa siku tatu kuondoka eneo hilo.

Gondwe alifanya ziara hiyo Jumapili jioni katika eneo la Mbuyuni, Kata ya Salasala na kuwataka wamachinga hao kuondoka na kuhamia katika eneo la Kisanga ambalo limetengwa kwa ajili yao.

"Ni jambo la kueleweshana na kuelekezana na sisi ni wazazi, kwa hiyo nimekuja kama Mkuu wa Wilaya, lakini kama mzazi, kusisitiza yale ambayo tulianza nayo kuwa tusiingilie maeneo ya taasisi za dini.

"Ile ni imani na imani huwa haichezewi, leo (Jumapili) wameshindwa kusali asubuhi sio jambo zuri kabisa na mmeona wenyewe," alisisitiza Gondwe.

Aliendelea kuhimiza, wafanyabiashara hao waelekee katika eneo lililotengwa na kupitishwa na serikali na viongozi wa wafanyabiashara hao.

Makamu Askofu wa Kanisa hilo la Bikira Maria, Jimbo la Dar es Salaam, Cleophace Bachuba, akizungumza na Nipashe baada ya agizo hilo, alimshukuru Mkuu wa wilaya kwa kufika eneo hilo na kuwaondoa wafanyabiashara hao.

Alisema tangu jana asubuhi wafanyabiashara hao walianza kuhamisha vibanda na mizigo yao waliyokuwa wameweka katika eneo hilo.

"Tunawashukuru watendaji wa Rais Samia Suluhu Hassan kuwa wasikivu, kusikia kilio chetu na kuja kututatulia kero hii. Vyombo vya habari navyo vimefanya kazi kuwa hasa gazeti la Nipashe, tunawashukuru sana," alisema Askofu Bachuba.

Wafanyabiashara hao waliokuwa wakifanya biashara zao kando ya barabara ya Bagamoyo eneo la Mbuyuni, baada ya kutakiwa kuondoka walivamia eneo hilo la kanisa na kuweka kambi.

Walihamishia, meza, mizigo na mabanda yao katika eneo hilo la kanisa hali iliyowafanya waumini wake kushindwa kuendelea na ibada.

Kabla ya agizo hilo, Nipashe lilishuhudia pia wafanyabiashara wakiwa wamezingira eneo la njia ya kuingia katika kanisa hilo, licha ya juhudi zilizofanyika za kuwaondoa na kujenga uzio upande mmoja.

Kwa mujibu wa Paroko wa Kanisa hilo, Padri Frumentios Msuri, eneo hilo walipatiwa na mmoja wa waumini wakajenga kanisa mwaka 1939 na wanaendesha ibada zao miaka yote.

SIMBA CEMENT
STRENGTH WITHIN

## INVITATION FOR TENDERS FOR SERVICES

1. Tanga Cement Public Limited Company Limited is hereby soliciting bids from interested eligible companies and individuals to render services listed in the schedule below for the year 2022.
2. Interested eligible bidders may obtain a complete set of bidding documents from the office of the Procurement Manager located at the Tanga Cement premises in Tanga between 08H00 and 14H00 hours on Mondays through Fridays (excluding public holidays).
3. Sealed bids must be deposited in the Tender Box located at the Tanga Cement visitors' gate in Tanga by 12H00 on the 30 November 2021.
4. Sealed tenders and modifications thereof must be deposited in the Tender Box located at the visitors' gate by 12H00 on the closing date indicated above. All tenders submitted must be valid for as specified in tender documents from the closing date indicated above. All tenders must be sealed, marked with the relevant tender title, and addressed to:

**The Managing Director**
Tanga Cement Public Limited Company
P O Box 5053
**Tanga** – Tanzania

5. This is a mere invitation to bids; it does not in any way constitute an offer to a contract or bind the Company.
6. Tanga Cement PLC is not bound to accept the lowest or any other bid.

| S/No. | Tender Tittle |
|---|---|
| 1 | Cement Loading Services |
| 2 | Staff transport services |
| 3 | Landscaping, Grass Cutting and General Cleaning Services |
| 4 | Off loading of Raw Materials |
| 5 | Supply and Administration of Casual Workers at Red Clay and Limestone Units |
| 6 | Yard Gang Administration Services |
| 7 | Office Cleaning Services |
| 8 | Plant Security Services |

216572202

# Wenye magonjwa ya damu kutambuliwa kitakwimu

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema itawatambua wagonjwa wote wenye magonjwa ya damu (Himofilia na selimundu) kwa kuwa na takwimu zao.

Lengo ni kuweka mipango ya namna bora ya kuwahudumia kwa sababu mgonjwa mmoja kwa mwaka inakadiriwa hutumia Sh. milioni 200.

Kaimu Mkurugenzi wa Magonjwa yasiyoambukiza kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. James Kiologwe, aliyasema hayo jana katika kikao kazi cha kwanza kati ya vitatu vinavyotarajiwa kufanyika baina ya Wizara ya Afya Tanzania na ya Kenya.

Wagonjwa hao wanakwenda kutambuliwa kupitia mradi wa kuongeza kasi ya upatikanaji wa huduma kwa wagonjwa wenye magonjwa ya damu ambapo vituo sita vya kuwahudumia vimeanzishwa katika Hospitali za Kanda na Mikoa.

Mradi huo unatekelezwa kwa ushirikiano wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na wadau afya ambao ni Taasisi ya Novo Nordisk Haemophilia (NNHF), Taasisi ya Novo Nordisk (NNF), Chama cha Himofilia cha Kenya(KHA), Chama cha Himofilia cha Tanzania (THA).

Akizungumza katika kikao hicho, Dk. Kiologwe alisema ugonjwa wa Himofilia una gharama kubwa ambapo sindano moja kwa mgonjwa ni Sh. milioni 20 hivyo kwa mwaka ni Sh. milioni 200.

"Sidhani kama kuna Mtanzania ambaye anaweza kumudu hizi gharama bila ya wadau hawa, ndiyo maana tumekutana hapa kupanga mipango yenye matumaini mapya kwa wagonjwa hawa. Leo tutaona namna mifumo ikakavyokwenda kuwatambua, hatutakuwa walegevu tunakwenda kuweka katika milango yetu ili kuwasaidia wagonjwa hawa wa Himofilia na selimundu," alisema.

Aliwataka wadau ambao watashiriki vikao hivyo mara baada ya kumalizika maazimio yake yawasilishwe serikalini ili iyafanyie kazi.

Katika hatua nyingine alimpongeza Mkuu wa Kitengo cha Magonjwa ya Damu Muhimbili, Dk. Stella Rwezaula kwa upekee wake wa kujituma na kuhakikisha mipango yote inayohusu wagonjwa hao inafanikiwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Muhimbili, Prof. Lawrence Museru kwa kuruhusu na usimamiaji.

Dk. Rwezaula ambaye ni msimamizi wa mradi huo Tanzania, alisema tangu uzinduliwe Novemba mwaka jana, kasi ya upatikanaji wa vituo vya kuhudumia wagonjwa hao ni kubwa.

Alisema kwa Tanzania mradi huo unatekelezwa kwa kuhakikisha kunakuwa na vituo sita vya huduma ambapo ni Kilimanjaro (KCMC), Mwanza (Bugando), Dodoma (Benjamin Mkapa), Dar es Salaam (Muhimbili), Mbeya na Morogoro (Hospitali ya Rufani).



Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Dastan Kyobya (wapili kulia), akikabidhi zawadi ya guta kwa mmoja wa washindi wa droo ya pili ya kampeni ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani' inayoendeshwa na Benki ya NBC kwa wakulima wa korosho mikoa ya Lindi na Mtwara, Shabani Mangoni ambaye ni Mwenyekiti AMCOS ya Kilomba iliyopo mkoani Mtwara, mwishoni mwa wiki.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakataa maji ya bomba wadai yana chumvi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga wamekataa kutumia mradi wa maji ya bomba kwa madai yana chumvi.

Mradi huo ulijengwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kwa gharama ya Sh. milioni 633.4 ili kuwaondolea wananchi adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta huduma ya majisafi na salama.

Wananchi hao wamekataa maji hayo na kuamua kuendelea kutumia ya visima vifupi vilivyochimbwa majumbani na kwenye majaruba ya mpunga ambayo yanasadikika kuwa siyo safi na salama kiafya.

Hayo waliyabainisha jana wakati wa mkutano wa nusu mwaka wa wadau wa maji na vyombo vya watoa huduma ya maji ngazi ya jamii kutoka Halmashauri za Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama chini ya RUWASA.

Mmoja wa wananchi hao, Simeo Henerico alisema, moja ya sababu ya kuacha kutumia maji hayo ni ladha ya maji hayo kuwa na chumvi.

Alisema tatizo lingine linalowafanya wananchi washindwe kutumia maji hayo ni gharama kubwa uniti moja sawa na lita 1000 wanauziwa Sh. 2,500.

Kaimu Meneja wa RUWASA Mkoa wa Shinyanga, Mnada Josephat, alisema Halmashauri ya Ushetu walichimba visima tisa vya maji, lakini kati ya hivyo saba vilikosa maji na visima viwili vilikamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Aidha, alisema ili kuondoa tatizo hilo kwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2021/2022, watatangaza mradi wa kupeleka maji ya Ziwa Victoria Ushetu kutokea Kijiji cha Nyamtukuza Halmashauri ya Nyang'whale, mkoani Geita.

Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timoth Ndaya, aliwaagiza wataalamu wa RUWASA kupima maji hayo kujua yana chumvi kiasi gani na kutoa elimu kwa wananchi hao ili waendelee kuyatumia.

Awali akisoma taarifa ya utekelezaji wa miradi ya maji, Kaimu Meneja wa RUWASA Kahama, Paschal Mnyeti alisema, mwaka wa fedha 2019/2020 kuanzia mwezi Julai, Oktoba walipokea Sh. bilioni 24.085 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi 16, Msalala, Ushetu na Manispaa ya Kahama na sasa miradi saba inatoa huduma.

# Wakulima korosho wavuna zawadi zaidi

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Mtwara, Dastan Kyobya, ameiomba Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kuangalia uwezekano wa kuongeza zaidi matawi yake katika mikoa ya Mtwara na Lindi ili kuwafikia zaidi wakulima wa korosho wa mikoa hiyo ambao wanahitaji huduma rafiki za kibenki.

Aidha, wakulima hao wakinufaika na kuvutiwa zaidi na huduma ya akaunti ya NBC Shambani inayotolewa na benki hiyo. Akizungumza mwishoni mwa wiki mkoani humo wakati wa kukabidhi ya zawadi mbambali kwa wakulima wa korosho mkoa wa Mtwara walioibuka washindi wa droo ya pili ya kampeni ya 'Vuna Zaidi na NBC Shambani', Kyobya alisema pamoja na kuhitaji huduma za kibenki zilizo karibu zaidi na maeneo yao wakulima wa korosho katika mikoa hiyo wanahitaji huduma zinazoendana na mahitaji ya kilimo cha zao husika.

"Mwitikio huu mkubwa unaoshuhudiwa sasa kwa wakulima wa korosho kujiunga zaidi na Benki ya NBC ni ushahidi tosha kwamba wakulima wanauhitaji zaidi na huduma zinazoendana na mahitaji yao. Jitihada hizi za NBC zimeonyesha kuunga mkono juhudi za wakulima na serikali katika kuboresha kilimo cha korosho katika mikoa ya Mtwara na Lindi," alisema.

"Pia zawadi zinazotolewa kupitia kampeni hii ikiwamo baiskeli, pikipiki, pampu za kupulizia dawa mikorosho, guta kama kanga, mabegi ya shule na madaftari ni ushuhuda tosha kwamba huduma hii kweli inalenga kuchochea kilimo cha zao la korosho vinginevyo mngeweza kuwapatia wakulima zawadi nyingine ambazo haziendani na mahitaji ya kilimo cha zao la korosho...hongereni sana," alisema.

Alisema kupitia mwitikio huo ipo haja ya benki hiyo kuongeza matawi yake, ikiwamo huduma ya uwakala wa kibenki katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo ili wakulima hao waweze kunufaika zaidi na huduma hizo zinazoambatana na mikopo ya zana za kilimo na ushauri wa kitaalamu kuhusu kilimo cha kisasa.

Aliwataka wakulima hao kutumia vifaa hivyo ipasavyo ili viweze kuwasaidia katika kuhakikisha wanaongeza uzalishaji wa zao hili kwa kujiandaa vema kwa ajili ya msimu ujao.

Meneja wa benki hiyo Kanda ya Kusini, Zubeider Haroun, alisema kupitia droo hiyo ya pili benki ilitoa zawadi za aina mbalimbali zipatazo 23 ikiwamo pikipiki 3, baiskeli 10, pampu za kupulizia dawa mikorosho 9, guta (Toyo)1, pamoja na zawadi za nyingine ikiwamo kanga, mabegi ya shule na madaftari kwa wakulima mmoja mmoja na AMCOS katika mikoa ya Mtwara na Lindi.

"Kampeni hii inalenga kusaidia jitihada zilizowekwa na serikali za kuongeza uzalishaji wa korosho kutoka tani 280,000 zinazozalishwa sasa hadi kufikia tani 700,000 ifikapo mwaka 2025 sambamba na kuwahamasisha wakulima wa korosho kufanya kazi kwa bidii ili kuongeza uzalishaji."

Kwa upande wao washindi wa droo hiyo waliishukuru NBC kwa kuandaa kwa kampeni hiyo kwa kuwa imekuwa na msaada mkubwa kwao.

## 500 wapewa wiki kuondoka eneo la uchimbaji

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

SERIKALI mkoani Geita imetoa siku saba kwa watu zaidi ya 500 waliovamia leseni ya uchimbaji madini ya kampuni ya Tanzos Mines Ltd katika kijiji cha Imwelu, wilayani Chato kuondoka eneo hilo.

Akizungumza na mwishoni mwa wiki ofisini kwake, Ofisa Madini Mkazi, mkoani humo, Daniel Mapunda, alisema baada ya siku saba walizopewa kumalizika hatua za kisheria zitafuatwa.

Alisema uvamizi huo umeathiri shughuli za maandalizi ya uanzishwaji mgodi huo baada ya kampuni hiyo kupewa leseni ya kuchimba dhahabu katika kijiji hicho.

"Serikali imetoa siku saba na muda huo unamalizika Jumamosi, kufikia wiki ijayo kila mvamizi anatakiwa kuondoka mwenyewe ili kupisha shughuli za mwekezaji kuendelea," alisisitiza Mapunda.

Alisema ofisi yake imeendelea kutoa elimu kwa wananchi waliovamia eneo hilo na kuanza uchimbaji madini kabla ya kuwataka kuondoka ikiwamo taratibu za kupata leseni na manufaa ya ujio wa mwekezaji huyo.

Aidha, wakazi wa maeneo yanayokusudiwa kujengwa mgodi huo wa kuchimba dhahabu na kampuni hiyo wametakiwa kutoa ushirikiano kwa Halmashauri ya Wilaya ya Chato na mwekezaji ili kufanyiwa tathmini ya mali zao na kulipwa fidia.

Mapunda aliongeza kuwa kampuni hiyo ipo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za kufungua mgodi wa dhahabu wa kati na mpaka sasa zaidi ya 200 wameshalipwa fidia kupisha ujenzi huo.

Akizungumzia uvamizi huo, mwakilishi wa kampuni hiyo, Naftael Mrutu, alisema uvamazi huo umeathiri shughuli za ujenzi wa mgodi ikiwamo kusitisha kwa muda kuletwa kwa vifaa vya kujengea miundombinu.

Kwa upande wake, msimamizi wa kambi ya Tanzos katika eneo hilo, Titus Kalori, alisema uvamizi huo ulifanyika mwezi uliopita baada ya watu wapatao 500 kuletwa na magari usiku kutoka maeneo tofauti na kuanza uchimbaji ndani ya leseni ya kampuni hiyo.

Akithibitisha kutokea kwa uvamzi huo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Imwelu, Seleman Buzegele, alisema kampuni ya Tanzos ilikiri kupata taarifa hizo.

# Majaliwa aipongeza Jumuiya Kihindu utoaji huduma kijamii

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameipongeza Jumuiya ya Kihindu nchini kwa mchango inaoutoa kwenye jamii hususan katika utoaji wa huduma za kijamii ikiwamo afya, elimu, maji, michezo na huduma za kiroho ambazo zimekuwa chachu kwa mshikamano na umoja.

Majaliwa alisema sambamba na suala hilo la kiroho, pia serikali inatambua mchango mkubwa unaotolewa na Shree Hindu Mandal kwa upande wa huduma za afya.

"Jambo lililonivutia zaidi kwenye eneo hilo ni kitendo cha hospitali zenu kupokea wagonjwa ambao asilimia 95 wanatumia bima ya afya ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)."

Majaliwa alitoa kauli hiyo juzi wakati alipomwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan katika maadhimisho ya Siku ya Diwali inayoashiria kuanza kwa mwaka mpya wa Kihindu 2078 (Vikram Samvat 2078), yaliyofanyika, Kisutu mkoani Dar es Salaam.

"Kama mnavyofahamu, serikali ina lengo la kuongeza wigo wa matumizi ya bima ya afya kupitia Mpango wa Bima ya Afya kwa Wote. Hatua za awali kuhusu mpango huo zimekamilika na katika bajeti ya serikali mwaka wa fedha 2022/2023, Mheshimiwa Rais Samia ameruhusu kutenga jumla ya Sh. bilioni 149.7 kwa ajili ya mpango huo".

Pia Waziri Mkuu ameihakikishia Jumuiya ya Kihindu Tanzania kuwa serikali inaendelea kuheshimu uhuru wa kuabudu kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na itaendelea kushirikiana nao pamoja na taasisi nyingine za kidini kwa ajili ya ustawi wa taifa na watu wake.

"Serikali inapongeza na kuthamini mchango wenu katika kujenga jamii yenye kutii mamlaka na sheria za nchi. Nitoe rai kwenu kutumia vema fursa ya uwapo wa kamati za amani kujadili pamoja na kuhakikisha kuwa nchi yetu inaendelea kuwa na amani na utulivu."

Alisema huduma ya kiroho imekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha amani, umoja na mshikamano nchini. "Nitumie fursa hii kuipongeza tena Taasisi ya Shree Sanatan Dharma Sabha kwa kuwekeza nguvu kubwa kwenye mafunzo ya kiroho hususan kwa jamii ya Wahindu nchini."

"Elimu mnayoitoa inawafikia vizuri waumini na wanaizingatia. Nataka niwakumbushe tena viongozi wote wa dini neno lenu ni muhimu sana, viongozi wa dini mnaaminiwa sana na ndiyo kwa sababu serikali inaendelea kuwaahidi kuwapa ushirikiano katika kusimamia mwenendo wa shughuli zenu na haitaingilia ila itashirikiana nanyi."

Aidha, Waziri Mkuu ameitaka jamii hiyo na Watanzania kwa ujumla kuendelea kuimarisha mshikamano ambao umejengwa kwa muda mrefu, wazidishe utu tulio nao, sambamba na kuwajali wajane na watu wengine wenye uhitaji.

Kwa upande wake, Rais wa Baraza la Wahindu Tanzania, Bhavin Borkhataria, alimpongeza Rais Samia kwa jitihada zake za kuiletea nchi maendeleo na kwamba wataendelea kumuunga mkono.

Pia kiongozi huyo aliiomba serikali isaidie Baraza la Wahindu Tanzania liweze kutambuliwa kwenye gazeti la serikali kwa kuwa ndiyo chombo chenye maamuzi ya juu kwa taasisi zote za kihindu zilizopo nchini.




Mshindi wa droo ya nne ya msimu wa pili wa kampeni ya Weka Akiba na Ushinde inayoendeshwa na Benki ya NMB 'Bonge la Mpango – 2merudi Tena', Richard Iranga (katikati), akiwasha pikipiki ya miguu mitatu baada ya kukabidhiwa katika hafla iliyofanyika viwanja vya stendi ya daladala Simu 2000 jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Meneja wa NMB Tawi la Mlimani City, Deogratias Kawonga na wapili kulia ni Meneja Uhusiano wa Amana za Wateja, Monica Job na Ofisa Mauzo, Regina Charles. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kilimo cha mpira chapigiwa chapuo na Bunge

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii imeomba serikali kuhamasisha kilimo cha mpira nchini ili kupata malighafi kwa ajili ya kiwanda cha kutengeneza dawa na vifaa tiba.

Agizo hilo lilitolewa jana na Mwenyekiti wa kamati hiyo, Stanslaus Nyongo, baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa viwanda vya kuzalisha dawa na vifaa tiba kilichopo Kijiji cha Idofi Halmashauri ya Mji wa Makambako, mkoani Njombe.

Alisema ili kiwanda hicho kiweze kuzalisha vifaa tiba ikiwamo mipira ya kuvaa mikononi ni lazima kuwapo na malighafi za kutosha ambazo zitafanya kiwanda kifanye kazi kwa ufanisi zaidi.

Vile vile, alisema kwa sasa kilimo cha zao la mpira kinatekelezwa katika maeneo ya pwani zaidi Tanga, Mtwara na Zanzibar na kwamba kuna haja ya kuhamasisha maeneo mengine kulimwa zao la mpira ili kukidhi mahitaji ya kiwanda hicho.

Nyongo alisema uamuzi wa ujenzi wa kiwanda hicho ulikuwa sahihi kwa kuwa kukamilika kwake kutatatua changamoto ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba ikiwamo mipira ya mikononi (glovu).

"Lazima tujipongeze na kujipa moyo tunaweza kuona ni kazi nyepesi kumbe ni ngumu kwani unaweza kupata hata maadui kwa kuwa wapo wanaosambaza gloves na dawa za watoto na vifaa tiba mbalimbali hawawezi kupenda kiwanda hiki kijengwe," alisema Nyongo.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Mwanaidi Ali Hamisi, alisema kiwanda hicho cha kutengeneza dawa na vifaa tiba kimegharimu Sh. bilioni 13.6 na ujenzi wake umefikia zaidi ya asilimia 90.

Alisema serikali itahakikisha inawajengea uwezo wananchi hususan wakulima ili waweze kuzalisha zao la mpira ambalo litatumika kama malighafi kwa ajili ya kiwanda hicho.

Alisema ili kurahisisha upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya kutengeneza mipira ya mikono wataomba nafasi ya kuonana na Rais Samia Suluhu Hassan ili naye azungumze na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, malighafi hizo zipatikane kwa haraka na kiwanda kianze kufanya kazi.

"Ni imani yangu mheshimiwa Rais atakubaliana na jambo hili kwani zao hili analijua huko nyuma alishawahi kuwa kwenye Wizara ya Kilimo," alisema Mwanaidi.

Mkurugenzi Mkuu wa Bohari ya Dawa (MSD), Meja Jenerali Dk. Gabriel Mhidze, alisema kiwanda hicho mpaka kukamilika kimejengwa kwa kushirikisha wataalamu ambao ni wazawa ili kupata ujuzi.

Alisema kiwanda hicho hakijaanza kufanya kazi kwa sababu wataalamu ambao ni wazawa walitakiwa kupelekwa nje ya nchi kujifunza namna ya kuchanganya dawa ya kutengeneza mipira ya mikono, lakini kutokana na ugonjwa wa Covid-19 ilishindikana.

Baadhi ya wajumbe wa kamati hiyo akiwamo Dk. Paulina Nahato na Husna Sekiboko, waliipongeza Wizara ya Afya kwa kubuni mradi wa ujenzi wa kiwanda hicho kwa kuwa mahitaji ya dawa na vifaa tiba nchini kwa sasa ni makubwa.

"Ipo haja ya wizara kuangalia njia mbadala ya kupata malighafi, lakini umeme wa uhakika kwani hali halisi ya umeme nchini inafahamika," alisema Husna.

# M/kiti asimamishwa kazi madai kutoza wananchi faini ya ng'ombe

**Na Shaban Njia,**
KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama mkoani Shinyanga, imemsimamisha kazi Mwenyekiti wa Kijiji cha Butondolo, Kata ya Isakajana Halmashauri ya Msalala, Mange Shilinde, kwa tuhuma za kuwapiga faini ya ng'ombe wananchi na walimu wanaopinga maamuzi yake kwa kushirikiana na jeshi la jadi (Sungusungu).

Kadhalika, anadaiwa kukodisha maeneo yote ya Shule ya Msingi Butondolo kwa wananchi bila idhini ya kamati ya bodi ya shule na fedha zinazopatikana anazitumia katika matumizi yake binafsi huku akiwalaghai wananchi kwamba fedha hizo zitatumika katika kutengeneza madawati ya shule.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alitoa uamuzi huo jana wakati wa mkutano wa hadhara kijijini hapo uliokuwa na lengo la kusikiliza kero mbalimbali zinazowakabili wananchi pamoja na kuzipatia ufumbuzi. Alisema, ofisa yake imekuwa ikipokea malalamiko mengi kuhusu mwenyekiti huyo hali iliyomlazimu kuitisha mkutano.

Akifafanua alisema, mwenyekiti huyo alibatilisha uamuzi wa ujenzi wa zahanati ya kijiji hicho iliyotakiwa kujengwa kwa nguvu za wananchi katika kitongoji cha Seseko na kulazimisha ujenzi ufanyike katika makao makuu ya kijiji cha Butondolo hali ambayo imesababisha wananchi kugoma kuchangia mchango wowote wa maendeleo.

"Mwaka 2016 wanakijiji walikubaliana kujenga zahanati katika kitongoji cha Seseko na kuchangia tofali 2,000, lakini Shilinde alipoingia madarakani alibatilisha maamuzi ya kijiji na kuamuru ujenzi ufanyike katika kitongoji cha Butondolo hali hii imesababisha wananchi kugoma kushiriki shughuli za maendeleo," alisema Kiswaga.

"Hatuwezi kuwa na viongozi wa vijiji Miungu watu wanaoendelea kunyanyasa wananchi vijijini na kusababisha kuwapo kwa migogoro isiyokuwa na tija na kwa mamlaka niliyonayo ninamsimamisha kazi na ninatoa onyo kwa viongozi wengine wa vijiji wenye tabia kama hizi," alisema.

Naye Diwani wa Kata ya Isakajana, Paschal Mlingito, alisema, wamekaa vikao kadhaa kumuonya mwenyekiti huyo, lakini hakutaka kusikiliza kiongozi yeyote, nakwamba uamuzi anaochukua hauwezi kuingiliwa na mtu yeyote hali iliyosababisha wananchi kugawanyika na kutoshiriki shughuli za maendeleo.

Awali, akijitetea mbele ya mkutano huo, Shilinde alisema tuhuma hizo sio za kweli na kwamba uamuzi wa kuhamisha ujenzi wa zahanati hiyo ulikuwa ni makubaliano ya mkutano halali ulioitishwa mwaka jana na wananchi kukubali kuhamisha ujenzi, lakini ulipoanza waligoma kuchangia fedha za ujenzi wa mradi huo.

Akijibu tuhuma za kuwatoza faini ya ng'ombe wananchi na walimu, alisema ni wale wanaowakamata wakiwa na makosa mbalimbali na sheria hizo zinasimamiwa na jeshi la jadi (Sungusungu) ambazo walijiweka wao wenyewe kijijini hapo.

Akizungumza kwa niaba ya wananchi, Nkwabi Bucheyebi alisema, wananchi hawakuwahi kufanya kikao chochote cha kubatilisha uamuzi wa ujenzi wa zahanati na kwamba ameufanya mwenyewe kwa kushirikiana na wajumbe wa serikali ya kijiji bila kushirikisha wananchi.

Alisema, katika kijiji chao kila wanapofaya mradi wowote wa maendeleo wanakaa na kukubali na kuanza kutekeleza, lakini baada ya kupatikana kwa mwenyekiti huyo anafanya uamuzi bila kushirikisha wananchi na unapopigwa faini ya ng'ombe na ukikaidi kutoa anaagiza utengwe na kijiji.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Emmanuel Tutuba (kushoto), akipewa maelezo kuhusu Benki ya Maendeleo TIB kutoka kwa Meneja Masoko na Uhusiano wa Kitaasisi wa benki hiyo, Said Mkabakuli (kulia), wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Huduma za Fedha kitaifa yaliyofanyika Viwanja vya Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam. Katikati ni Kamishna wa Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha na Mipango, Dk. Charles Mwamwaja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi mgeni rasmi kongamano wataalamu wa bima

**Na Christina Mwakangale**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anatarajia kuwa mgeni rasmi katika kongamano la mashirika na wataalamu wa bima kutoka barani Afrika litakaloanza Januari 26 hadi 28, mwakani, visiwani humo.

Kongamano hilo ambako litashirikisha washiriki takribani 300 limeandaliwa na Chuo cha Afrika cha Bima na Hifadhi ya Jamii (ACISP) pamoja na Jukwaa la Wamiliki wa Kampuni za Bima (ICFT) na Chama cha Bima Tanzania (ATI).

Mwenyekiti wa ICFT na kamati ya maandalizi ya kongamano hilo, David Sawe, akizungumza mwishoni mwa wiki, alisema mkutano huo wa watendaji wakuu na wataalamu wa hali ya juu umewekwa kama kikao cha kutafakari mkakati wa tasnia ya bima barani Afrika.

"Mada zitakazozungumzwa zitahusisha bima za kilimo, afya na matibabu, maisha, rasilimali watu na utaalamu wa sekta ya bima. Katika siku hizi tatu, wajumbe watatafakari juu ya maendeleo ya tasnia kutoka kwa utendaji hadi mitazamo ya sera," alisema Sawe.

Kadhalika, alibainisha kwamba, washiriki majadiliano ya ndani na kikao cha mkakati, kufanya mafunzo ya wakurugenzi kwa bodi za wakurugenzi za kampuni za bima zinazohudhuria, kama zinavyoungwa mkono na Shirika la Afrika Reinsurance na kufungua ikiwamo kufurahia vivutio vya utalii visiwani Zanzibar.

Sawe, alifafanua kwamba, mkusanyiko huo wa watendaji wakuu na wataalamu wa hali ya juu umewekwa kama kikao cha kwanza cha mazungumzo na mkakati wa tasnia barani Afrika.

Alisema kongamano hilo ni muhimu na wahudhuriaji watakuwa kutoka nje na ndani ya Tanzania, wakijumuisha ICFT, ATI, TIBA, Bancassurers, Mobile Network Operators.

(MNOs), InsurTechs/Fintechs, washirika wa Maendeleo na Mamlaka ya Udhibiti wa Bima (TIRA) pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango.

Vilevile, Sawe alibainisha kwamba, wadau wa mifuko ya pensheni, masoko ya hisa na mitaji watashiriki na pia kongamano hilo limepangwa chini ya falsafa ya tafakari, ushirikiano na maoni kwa viongozi na watendaji wa tasnia ya bima.

# Mchimbaji alivyofariki kwa kuangukiwa na mwamba

**Na Deogratius Nsokolo,**
KIBONDO

MTU mmoja aliyetambulika kama Ntibilile Bahutunze, amefariki dunia na wengine watatu kunusurika baada ya kufukiwa na udongo wa mwamba wa madini aina ya chokaa katika Kijiji cha Kasebuzi, wilayani Kibondo mkoani Kigoma wakati wakichimba madini hayo.

Walionusurika pamoja na wachimbaji katika mgodi huo wamesema tukio hilo lilikuwa la ghafla na walishindwa kumwokoa kutokana na miundombinu duni na zana za kusaidia uokoaji.

Mmoja wa walionusurika kwenye tukio hilo, Magambo Kagoroba, alisema walianza kuona dalili za udongo kuanza kudondoka kidogo kidogo na wakawahi kutoka ndani ya shimo, lakini mwenzao Bahutunze alibaki na alipojaribu kujiokoa baadaye alishindwa baada ya mwamba wa madini hayo kumwangukia na kumfunika.

"Tulijitahidi kutaka kumsaidia mwenzetu ambaye alikuwa bosi wetu, lakini hatukuweza kutokana na kutokuwa na zana na hata greda lilipokuja baadaye tayari alikuwa ameshakufa," alisema Matenga Honori, mmoja wa walionusurika.

Walisema hii ni mara ya pili kwa tukio kama hilo kutokea na kuiomba serikali na wamiliki wa migodi hiyo kuweka vifaa vya kisasa vinavyoweza kuwasaidia kwa haraka linapotokea tukio la namna hiyo.

Mkuu wa Wilaya ya Kibondo, Kanali Agrey Magwaza, alisema serikali imepokea kwa masikitiko tukio hilo ambalo majeruhi wanaendelea na matibabu.

Alisema baada ya kupata taarifa walipeleka msaada mara moja kwa ajili ya kuondoa kifusi na kuokoa maisha ya mchimbaji aliyebaki ndani, lakini haikusaidia.

Alisema serikali ya wilaya inatafakari kuona namna bora ya kuweka mazingira salama kwa wachimbaji katika wilaya hiyo.

Nipashe

TESA

Jumanne Novemba 16, 2021

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 13



Ukurasa 12

## Wananchi wanavyoinua kijiji kielimu



## Ujenzi huu wa madarasa 15,000 unaandika historia sekta ya elimu

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

# WATAALAMU: BWAWA NYERERE YAJAYO YANAFURAHISHA

## ▪ Kuongeza maji Pwani, Dar es Salaam
## ▪ Kwaheri mafuriko ukanda wa Rufiji

MRADI wa kuzalisha umeme wa maji katika bwawa la Julius Nyerere ulianza kujengwa Desemba 2018 umebakiza takribani miezi saba kukamilika, ifikapo Juni 2022, lakini pamoja na kuongeza umeme mwingi kwenye gridi ya taifa, umewahi kuwaza kuna faidi nyingine?

Hivyo wakati kazi ya kujenga bwawa hilo linalogharimu Sh. trilioni 6.558 ikielekea ukingoni, Wizara ya Nishati inaainisha faida Watanzania wanazotarajia kuzivuna.

Kongamano la kujadili sera kuhusu faida zitokanazo na mradi wa bwawa la kuzalisha umeme wa Julius Nyerere, lililofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam, lina majibu, likitaja baadhi ya faida kama kulipatia taifa umeme wa uhakika.

Oscar Kashaigili Mkurugenzi Msaidizi Ufuatiliaji na Tathmini , Idara ya Sera na Mipango kutoka Wizara ya Nishati, anasema kukamilika kwa ujenzi huo kutaongeza megawati za umeme 2,115, katika gridi ya taifa, lakini umezalisha ajira 8,600 kati ya hizo 7,700 ni za Watanzania.

Mradi huo umeboresha shughuli za utalii katika pori la akiba la Selous na kuweka mazingira mazuri kwa wanyama kutokana na upatikanaji wa maji kwa kipindi chote cha mwaka mzima, anasema Kashaigili.



Mwonekano wa bwawa la kuzalisha umeme la Julius Nyerere. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

"Tumeongeza pato la taifa kutokana na ongezeko la shughuli za utalii katika eneo la mradi, pia uwekezaji na uzalishaji katika sekta nyingine kama vile kilimo umeongezeka." Anasema na kuongeza kuwa utasaidia pia kupunguza madhara ya mafuriko katika eneo la chini la Mto Rufiji.

Aidha, ujenzi wa mradi huo umeongeza pato la taifa kutokana na kuongezeka shughuli za utalii na michezo mbalimbali na kwamba kampuni binafsi zina nafasi zaidi ya kuuza bidhaa na kutoa huduma mbalimbali kwa mkandarasi na hivyo kuongeza pato la taifa na kutoa ajira kwa vijana na wanawake.

Kashaigili, anasema katika eneo hilo kuna maji mengi ambayo yametengwa kwa ajili ya uvuvi na kuongeza kuwa hiyo ni fursa kwa maendeleo ya kilimo na ufugaji wa samaki wa aina mbalimbali.

"Shughuli za kijamii na kiuchumi zinazofanyika katika eneo la juu la mradi zinaweza kuhama na kufanyika sehemu ya chini ya mradi na hivyo kuboresha upatikanaji wa maji katika bonde la Mto Rufiji, na Kibiti na hivyo kuendeleza sekta ya kilimo kwa maeneo mengi ya mkoa wa Pwani na Wilaya ya Kilwa katika mkoa wa Lindi." Anasema Kashaigili.

Maji yatakayotoka kwenye kufua umeme mwelekeo wake mkubwa ni mikoa ya Pwani na Dar Es Salaam na kwamba mito mitatu ya Ruvu, Wami na Rufiji itajumuisha pamoja maji yake na kuongeza wingi wa maji mikoa hiyo, mradi ukikamilika, anasema Kashaigili.

Aidha, anagusia fursa nyingine zinazoibuka kuwa ni pamoja na viwanda hasa vya kuchakata na kutengeneza bidhaa mbalimbali kutokana na kuwapo umeme na maji ya kutosha na kwa gharama nafuu.

Kuuza umeme wa ziada ni faida mojawapo, akieleza kuwa kutokana na ziada ya umeme itakayopatikana, Tanzania inaweza kuziuzia nishati nchi nyingine mfano za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na zile za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), Kwan mujibu wa Kashaigili.

Anaeleza washiriki kuwa kwa sasa kazi ya kufunga njia kuu za uzalishaji umeme imefikia asilimia 55.6. hivyo serikali inazihimiza wizara za kisekta zinazohusika na mradi huu kufanya tathmini ya kina kuhusu manufaa ya fursa hizo, ili zije na programu maalum za kimaendeleo kwa Watanzania.

"Ni muhimu kuanza kupanga na kuweka bajeti kwa ajili ya maendeleo ya fursa zitakazokuwa zimebainishwa." Anakumbusha.

**KUDHIBITI MAFURIKO**

Akiwasilisha mada katika kongamano hilo, Prof. Honest Ngowi, kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe anasema, baada ya kupitia miradi kama hiyo mitatu duniani, amebaini kuwa kuna manufaa mengi ya bwawa hilo kuanzia mwanzo hadi kukamilika.

"Kiasi cha maji kitakachoruhusiwa kuingia eneo la chini yatakuwa yale yaliyotumiwa kufua umeme, ni dhahiri kuwa kiasi kikubwa kinachohifadhiwa kwenye bwawa kinachoruhusiwa hakiwezi kuleta mafuriko eneo la chini lenye tambarare," anafafanua.

Amezitaja faida hizo kuwa ni pamoja na kudhibiti mafuriko, kufanikisha kilimo cha umwagiliaji, na kuongeza maji kwa ajili ya viwanda na matumizi ya nyumbani.

"Mbali na kuzalisha umeme, kutoa maji, na kilimo cha umwagiliaji, mradi huo unatoa ajira za moja kwa moja na ambazo siyo za moja kwa moja zaidi ya 8,600."

Naibu mwidhinishaji wa mfuko wa maendeleo wa Ulaya (European Development Fund EDF), Jonathan Mpuya, anasema ni muhimu wadau tofauti wakajua faida za mradi wa bwala la kuzalisha umeme la Julius Nyerere ili waweze kushiriki kikamilifu kuibua fursa na kuwekeza

INAENDELEA UK.12

ELIMU
NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Wananchi wanavyokiinua kijiji kielimu

## ■Watoa uwanja, nguvu kujenga shule

UMBALI mrefu kutoka zilipo shule hadi kwenye makazi ya wanavijiji umekuwa ni kikwazo kimojawapo kinachowarudisha nyuma wanafunzi kitaalamu hasa wanaosoma sekondari za kata.

Wanafunzi hasa mabinti huishia njiani kutokana na kuchoka kutembea kilometa nyingi kwenda na kurudi nyumbani wengine wakiwa na njaa, aidha kukumbana na vishawishi njiani vya lifti za bodaboda, usafiri binafsi na mafataki wanaowahadaa kuwapatia pesa za kumaliza matatizo yao.

Ni tatizo linalowakabili pia wanafunzi wa Kijiji cha Mmangu wilayani Shinyanga, wanaotembea zaidi ya kilomita 20 (kwenda na kurudi) ili kuifikia Sekondari ya Kata ya Salawe.

Ofisa Elimu, Kata ya Salawe, Joseph Kulwa, anasema wanakijiji wa Mmangu wana mpango wa kuanzisha sekodari kwenye kijiji hicho kwa nguvu za wananchi kuwaondolea kero watoto wao.

Anasema wananchi kwa nguvu zao wametoa uwanja, kuanza ujenzi na kukamilisha madarasa sita, ofisi ya walimu na matundu nane ya vyoo, wakitarajia wanafunzi kuanza kuitumia shule hiyo mwakani kwa kidato cha kwanza.

"Mmangu tuna wanafunzi wengi wanaokwenda kidato cha kwanza, mfano kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka huu waliofaulu kuingia kidato cha kwanza katika Sekondari ya Salawe ni 477 kati yao 280 wanatoka Mmangu," anasema Kulwa.

Anaeleza kuwa kukamilika shule hiyo kutaondoa msongamano wa wanafunzi katika shule nyingine za kata na kupata unafuu na hata ufaulu zaidi, anaongeza Kulwa.

Mwanakijiji cha Mmangu, Sekei Makonge, anasema wazo la kujenga shule hiyo limekuja kuwaondolea tatizo la umbali mrefu wa kutembea hadi shuleni, wanafunzi wengi wakiwamo wadogo wanaosoma shule za awali.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, (kulia), akiwa ziarani kuangalia ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Mmangu na vyumba vya madarasa matatu, (kushoto) ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Nice Munissy. **PICHA: MARCO MADUHU**

Anasema hali hiyo imewaumiza wasichana wanaopata ujauzito huku wengine wakikatisha masomo na kuolewa ndoa za utotoni, yote hayo yakimrudisha nyuma binti kufikia malengo yake kielimu.

"Kijiji chetu kipo mbali sana na shule ya kata, watoto wanasumbuka kwenda shuleni na wengine kukwamishwa na mambo mbalimbali, kuanzia udhaifu, njaa, kupata na kupata ujauzito hasa wasichana," anasema Makonge.

> "Mmangu tuna wanafunzi wengi wanaokwenda kidato cha kwanza, mfano kwenye matokeo ya darasa la saba mwaka huu waliofaulu kuingia kidato cha kwanza katika Sekondari ya Salawe ni 477 kati yao 280 wanatoka...

Zebedayo Shija anayeishi Kijiji cha Mmangu, anasema umbali mrefu unawakatisha tamaa wanafunzi wengine wanaokwamia njiani hasa maeneo yenye vichaka na misitu ambayo inaweza kuwa na wanyama wakali.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Nice Munissy, anasema wamepokea Shilingi bilioni 1.3 za kujenga madarasa 65, yakiwamo matatu ya Sekondari ya Mmangu.

Anaahidi kuwa pamoja na kuwapo madarasa, atahakikisha walimu wanakuwapo wa kutosha pamoja na vifaa vya kufundishia shuleni hapo.

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anapongeza wananchi wilayani humo kwa mstari wa mbele kujitolea kuchangia maendeleo kwa kuanzisha ujenzi wa maboma ya madarasa na kuyamaliza kwa nguvu zao.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, anafanya ziara ya kutembelea shule hiyo mpya ya Mmangu ili kuona maendeleo ya ujenzi wa vyumba vya madarasa matatu, ambayo Sh. milioni 60 zimetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Anasema ujenzi wa madarasa utayaongeza hadi kufikia tisa pamoja yakichanganywa na sita ambayo yamejengwa kwa nguvu za wananchi.

Aidha, Mjema anawapongeza wanakijiji cha Mmangu kwa kuguswa na taaluma za watoto wao, na kuamua kujenga shule mpya ya sekondari, jambo ambalo linapaswa kuigwa na wengine.

"Kwa vile wananchi mlijenga shule hii mpya ili kuwanusuru wasichana na mimba za utotoni nawashauri mjenge hosteli au mabweni, sababu mazingira ya huku naona bado si rafiki kwao kuna pori na vichaka, hivyo ni bora wakabaki hapa hapa shuleni, na sisi serikali tutawaunga mkono," anaongeza Mjema.

Mkuu huyo wa mkoa, anawaonya wanaume wilayani humo waache tabia ya kuwa na uhusiano na wanafunzi wawaache watimize ndoto zao na kuwataka watafute watu wazima na atakayebainika kumpatia ujauzito mwanafunzi, sheria itamshughulikia kikiwamo kifungo miaka 30 jela.

Takwimu za kitaifa za mwaka 2012, zinaitaja Shinyanga kuwa inaongoza kwa mimba na ndoa za utotoni kitaifa kwa asilimia 59, ikifuata Tabora asilimia 58, Mara ni ya tatu asilimia 55.

Wasichana wamekuwa wakiolewa au kupata ujauzito chini ya umri wa miaka 18 na kuvurugikiwa na utaratibu wa maisha.

# BWAWA NYERERE YAJAYO YANAFURAHISHA

INATOKA UK.11

katika maeneo mbalimbali ya kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

"Ndiyo maana serikali inaweka mazingira rafiki na wezeshi ili sekta binafsi iweze kushiriki kikamilifu, jamii na wakulima wadogo wadogo, wanawake na vijana wanaozunguka eneo lile nao waweze kunufaika na shughuli za uzalishaji," anasema Mpuya.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Amina Khamis Shaaban, anasema majadiliano ya kujadli sera kuhusu faida zitokanazo na mradi wa bwawa la kuzalisha umeme wa Julius Nyerere ni sehemu ya utaratibu na mkakati wa maendeleo unaosimamiwa na wizara hiyo.

Anawaambia washiriki kuwa utaratibu huo unatekelezwa kwa muda wa miaka nane mpaka 2025 na unakwenda sambamba na dira ya taifa ya maendeleo ya 2025.

Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, anasema mradi huu wa bwawa la kuzalisha umeme ukikamilika Watanzania wategemee faida nyingi ikiwamo upatikanaji wa umeme wa uhakika na wa bei nafuu na ajira kwa vijana na kina mama.

Profesa Mkenda anataja faida nyingine kuwa ni pamoja na utalii ulioboreshwa na uboreshaji shughuli za kilimo.

Desemba 2018 serikali ilisaini mkataba na mkandarasi M/S JV Arab Contractors & Elsewedy Electric, wa miezi 42 (miaka mitatu na miezi sita) , unaohusisha miezi sita ya maandalizi na miezi 36 (miaka mitatu) ya ujenzi wa bwawa hilo.

Utekeleza mkataba ulianza Desemba 2018 na unatarajiwa kumalizika Juni, 2022 na katika kazi hiyo mkandarasi ameshapokea Shilingi trilioni 2.99 sawa na asilimia 45.6 ya malipo yote yenye thamani ya Shilingi trilioni 6.558.

ELIMU
NA REUBENI LUMBAGALA

# Aina hii ya ujenzi madarasa 15,000 inaandika historia sekta ya elimu

VYUMBA vya kutosha vya madarasa, madawati, vyoo vinavyozingatia mahitaji ya kijinsia, maktaba na vitabu kwa uwiano wa mwanafunzi mmoja au wawili, maabara bila kusahau walimu wa kutosha ni mahitaji muhimu na ya lazima yanayowahakikishia wanafunzi mazingira ya elimu bora.

Vikikosekana hivyo ni tatizo wanalokumbana nalo walimu na wanafunzi . Wakati huu katika ngazi zote za elimu, kuanzia msingi, sekondari, vyuo vya kati na vya elimu ya juu, kumekuwa na ongezeko kubwa la udahili wa wanafunzi wanaojiunga na taasisi hizo za elimu.

Ongezeko hilo hasa wanafunzi wanaojiunga darasa la kwanza kwa shule za msingi na kidato cha kwanza kwa sekondari limezalisha mahitaji mbalimbali kama vile vyumba vya madarasa, vitabu, madawati, viti, meza, vyoo, mabweni, viwanja vya michezo, mabwalo, ofisi, nyumba za walimu, maktaba na maabara .

Yote haya yanatokana na serikali kugharamia elimu msingi kuanzia darasa la awali hadi sekondari.

Changamoto hizo zinaipa serikali na wadau wengine wa elimu jukumu la kuzitafutia ufumbuzi ili kuwa na mazingira wezeshi ya ufundishaji na ujifunzaji wenye tija kwa maendeleo ya wanafunzi, jamii na taifa pia.

Tanzania imepata mkopo wa masharti nafuu wa Shilingi trilioni 1.3 kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya kupambana na ugonjwa wa COVID-19 na wataalamu wake wameandaa andiko la namna ya kutumia fedha hizo na kuonyesha namna ambayo sekta mbalimbali zitaguswa kupitia mgawo wa fedha na tija ya mapambano itaonekana.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kushoto), katika moja ya ziara za kukagua ujenzi wa madarasa ya sekondari. **PICHA: MTANDAO**

Wizara za Afya, Maji, Elimu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Utalii zimeguswa moja kwa moja katika mgawo wa fedha hizo ili kuongeza kasi ya mapambano ya kuukabili ugonjwa huo unaoshambulia mfumo wa upumuaji.

Wizara ya Elimu imeibua suala la vyumba vya madarasa, madawati, meza na viti kuwa limekuwa kubwa hasa kwa shule za msingi na sekondari na kusababisha mrundikano wa wanafunzi katika darasa moja na wengi kukaa chini.

Moja ya visababishi vinavyoeneza au kusambaza kwa kasi maambukizi ya ugonjwa wa corona ni msongamano ndiyo maana wataalamu wa afya wanashauri kuepuka misongamano isiyo ya lazima ili kupunguza kuenea kwa maradhi hayo, hali hiyo inadhihirisha kuwa msongamano darasani si jambo jema.

Kwa hiyo, kama serikali isingefanya juhudi za kuongeza kasi ya ujenzi wa madarasa, wanafunzi pamoja na walimu wao wangekuwa katika hatari kubwa ya kuambukizwa COVID-19 kutokana na msongamano darasani.

Hivyo, ujenzi wa madarasa 12,000 kwa shule za sekondari na madarasa 3,000 kwa shule za msingi utafanikisha kupunguza hatari ya wanafunzi na walimu kuambukizwa COVID-19 wawapo shuleni wakati wa kujifunza na kufundishwa.

Kwa mujibu wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu, anapozungumza na wanahabari kuhusu mpango wa matumizi ya fedha za mapambano dhidi ya corona, anasema mahitaji ya vyumba vya madarasa kwa shule za sekondari ni 20,535, huku idadi ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga kidato cha kwanza mwakani ni ikifikia 1,022,936.

Kwa hiyo, wahitimu wa kidato cha nne mwaka huu wataacha madarasa 8,535 watakamaliza masomo kwa ngazi hiyo, hivyo ujenzi wa madarasa mapya 12,000 pamoja na madarasa 8,535 yatakayoachwa na wahitimu wa kidato cha nne, utawezesha wanafunzi wa kidato cha kwanza kusomea katika vyumba vya madarasa bila tatizo.

Anasema kutakuwa na madarasa 20,535 yatakayopatikana kwa kuongeza madarasa mapya 12,000 na 8,535 yatakayoachwa na wahitimu wa kidato cha nne.

Mradi wa ujenzi wa madarasa 15,000 ni mradi wa kihistoria katika sekta ya elimu kwani mradi huu unamaliza changamoto ya vyumba vya madarasa kwa shule za sekondari kwa kiwango kikubwa.

Ujenzi huo unapunguza changamoto ya madarasa kwa shule za msingi, maagizo ya Waziri Ummy kwa watendaji ni kwamba ifikapo Desemba 15, mwaka huu, ujenzi wa madarasa yote uwe umekamilika kwa nchi nzima.

Aidha, pamoja na utatuzi wa changamoto ya vyumba vya madarasa kwa shule za sekondari na kupunguza changamoto hiyo kwa shule za msingi, bado yapo matatizo mengine mengi yanayoikabili sekta ya elimu hasa kwa shule za msingi na sekondari.

Mahitaji hayo ni kama walimu, vitabu, mabweni, maabara, maktaba, mabwalo, nyumba za walimu, vyoo vya walimu na wanafunzi.

Hivyo, serikali ijitahidi kupunguza changamoto hizi kwa kushirikisha sekta binafsi na wadau wengine ili sekta ya elimu iweze kuwa na mazingira bora ya ujifunzaji na ufundishaji.

Uwepo wa mazingira bora ya ujifunzaji na ufundishaji unaongeza shauku ya wanafunzi kwenda shule na kujifunza, huku walimu wakiwa na morali ya kufanya kazi.

Wanafunzi na walimu kwa pamoja wakiwa katika mazingira mazuri na tulivu, hizo ni hatua za kuifanya kazi ya ujifunzaji na ufundishaji kufanyika kwa mafanikio makubwa na hata kufanikisha ufaulu na maendeleo ya taaluma kuongeza kwa kasi kubwa.

**Mwandishi ni Mwalimu wa Sekondari Mlali iliyoko Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.**
**Mawasiliano: 0620-800462.**

TEKNOLOJIA
NA SABATO KASIKA

# Ni enzi za kutuma 'SMS' kuzima taa, jokofu, kiyoyozi



Mkurugenzi wa TANTRADE, Latifa Mohamed (wa pili kushoto), akiangalia teknolojia inavyofanya kazi. Kushoto ni Mkuu wa chuo hicho, Prof. Emmanuel Mjema.
**PICHA: MTANDAO**

ZAMA hizi huna haja ya kuogopa au kuhofu kuwa hujazima taa za umeme, kiyoyozi au jokofu, kwasababu kwakutumia ujumbe wa simu ya mkononi unaweza kuzifikia na kuzizima, hata ukiwa nje ya mkoa unapoishi.

Mfumo huo unaoitwa Home Automation System, unaweza kufanyakazi mahali popote ikiwa kuna mtandao wa mawasiliano (network), na kwamba huunganishwa katika njia ya umeme unaokwenda kwenye vifaa vya umeme ndani ya nyumba mfano taa, jokofu na viyoyozi.

Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), cha jijini Dar es Salaam ni miongoni mwa wabunifu wanaotengeneza mfumo huo wa kuzima vifaa vya umeme kwa kutumia ujumbe wa simu (SMS).

Mhitimu wa chuo hicho ambaye ni mtaalamu wa teknolojia ya mawasiliano (IT), Ibhram Mzanda, anasema mfumo huo unaweza kupokea ujumbe na kutafsiri kila ambacho mhusika anataka kukifanya iwe ni kuwasha au kuzima kifaa chake japo hayupo nyumbani.

"Mfumo huo unaunganishwa na laini ya simu maalum kwa ajili ya kuzima au kuwasha vifaa hivyo. Kama ni taa unaandika washa balbu au zima, ukituma ujumbe utaeleza kuzima au kuwasha," anasema Mzanda.

Anafafanua kuwa mfumo huo unafanya kazi hata kama mtu atakuwa mbali na nyumbani kwake iwapo amesahau kuzima mojawapo ya vifaa vyake.

"Kama ukiandika kinyume na kile ambacho hukukusudia, ujumbe hauwezi kwenda, hivyo ni muhimu kila kifaa kuwa na ujumbe wake ili unapohitaji kuwasha au kuzima basi unatafuta sehemu husika," anasema.

Kutumia utaalamu huo kunadhihirishwa kwenye kongamano la 57 la kitaaluma chuoni hapo lililofanyika chuoni hapo wiki iliyopita.

Mgeni rasmi akiwa ni Mkurugenzi wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara (TANTRADE), Latifa Mohamed, anayekipongeza chuo hicho kwa ubunifu mkubwa kwenye nyanja mbalimbali za kitaaluma hasa maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Mkurugenzi huyo ambaye alisoma katika chuo hicho, anaingia na kofia ya mwanafunzi wa zamani wa chuo hicho lakini Mkurugenzi wa TANTRADE, anasema ameshangazwa na ubunifu wa wanafunzi wanaosoma TEHAMA chuoni hapo, kwa namna walivyobunifu mfumo unaomwezesha mtu kuzima taa au kifaa chochote cha umeme kwa kutumia simu.

"Mfano, kama umesahau kuzima mashine ya kufulia nguo, au kifaa chochote kinachotumia umeme kupitia ubunifu huu unaweza kuzima kwa kutumia simu yako ya mkononi ukiwa popote pale," anasema Latifa.

Anasema, hayo si maendeleo madogo katika teknolojia, bali ni makubwa ya kujivunia na kwamba chuo kimepiga hatua kubwa katika nyanja mbalimbali za kiteknolojia, tofauti na enzi hizo alipokuwa anasomea kozi ya masoko.

"Nimesoma hapa kozi ya masoko, hivyo nina ushuhuda wa maendeleo makubwa yaliyofikiwa chuoni hapa CBE. Chuo kimeona umuhimu wa kutumia teknolojia, natoa wito kwa Watanzania wote wawalete watoto wao hapa kwani kuna kozi zinazokwenda na wakati kwenye soko," anasema.

Katika hotuba yake, mkuu wa chuo hicho, Profesa Emmanuel Mjema anasema, wahitimu wa CBE, wamekuwa na uwezo wa kufanya mambo makubwa maeneo yote wanayokwenda kufanya kazi hali ambayo inakipandisha chuo hicho kwenye hadhi ya vyuo vikuu duniani.

"Tuko vizuri, ninawaomba mjidai na mtembee kifua mbele, kwani tufanya mambo makubwa kitaaluma, na kuna watu wanaulizia fulana za CBE zinapatikana wapi wakanunue sasa ukishaona watu wanataka kujinasibisha na wewe ujue mambo yako ni mazuri sana," Prof. Mjema anasema.

Anaongeza kuwa, kwa kawaida mtu ukiwa na pesa au maisha mazuri kila mtu atasema yule ni ndugu yangu, na kwamba akiwa hana kitu ama mwizi hakuna atakayependa kujinasibisha naye.

"Lakini sisi CBE kwa sasa watu wanapenda waonekane wako nasi kwa sababu wanaona tunafanya mambo yetu vizuri kuanzia kukuza teknolojia na ubunifu wa vitu mbalimbali," anasema.

Prof. Mjema anaahidi kuwa chuo hicho kitaendelea kufanya makubwa kuanzia kwenye utafiti kwa lengo la kujitofautishe na vyuo vingine ambavyo vimekuwa vikifanya mambo ya kawaida kwenye jamii.

"CBE imekuwa ikifanya vizuri kwa kuandaa na kufanya utafiti mbalimbali na kutoa machapisho ya kitaaluma ambayo yamekuwa na msaada kwenye ufundishaji," anasema.

Profesa Mjema anasema, wanafunzi chuoni hapo wamekuwa wakibuni vitu mbalimbali, lakini inashangaza kuona chuo bado hakijatangaza ubunifu huo ambao iwapo utaingizwa kwenye mashindano wanaweza kuibuka washindi.

"Katika katika mikutano ya kimataifa ya utafiti, CBE imekuwa ikishika nafasi ya kwanza kila mara kutokana na kuwa na maandiko na utafiti bora kuliko vyuo vingine vingi," anasema bila kufafanua maandiko hayo.

Anasema, mafanikio yote hayo ni muhimu wayatangaze ili yawafanikishe kujulikana duniani kwa kuwa hiyo mikutano ya kimataifa ya utafiti siyo ya Tanzania pekee bali kuna mataifa mengi yanahudhuria.

Anasema, amekuwa akisikia jinsi ambavyo watu wengi wanasifia chuo hicho kuwa ni bora zaidi, lakini bahati mbaya wanajumuiya ya CBE ni kama wanyonge, hawatambi inavyotakiwa kutokana na makubwa waliofanya.

"Ni lazima tujivunie vitu vyetu na tuvionyeshe kunapokuwa na makongamano kama haya, tuyatangaze mambo mazuri yanayofanywa, kwani ni mengi ila bado hayajafahamika ipasavyo kwa jamii ya Watanzania," anasema.





## Aeleza sababu miti inayopandwa kukauka

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Tawala Mkoa wa Dodoma, Fatma Mganga, amesema kuwa miti mingi inayopandwa katika Mkoa wa Dodoma inakufa kwa sababu ya kutokuwa na uangalizi baada ya kupandwa.

Akizungumza jijini hapa katika zoezi la upandaji miti lililoratibiwa na Taasisi ya Habari Development Association wakishirikiana na Stanbic Bank katika Shule ya Msingi Nala, alisema kila mwaka kumekuwa na siku maalum ya upandaji miti, lakini haistawi kutokana na kukosa matunzo.

"Tumegundua kwamba ina changamoto ya ufuatiliaji katika miti tunayo panda kwani hali halisi inaonyesha kuwa baada ya kupanda miti imekuwa ikitelekezwa hali inayosababisha kutostawi.

"Hivyo basi niwatake walimu wa Shule ya Msingi Nala kuhakikisha miti hiyo 1,200 iliyopandwa leo (jana) ambayo ni ya matunda na kivuli inastawi kwa kuwapa majukumu wanafunzi wenu kila mmoja kuwa na mti wenye jina lake ili kila mwanafunzi awe na hamasa ya kutunza mti wake," alisema.

Kwa upande wake Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambaye alikuwa mgeni rasmi katika upandaji miti, Philip Mangula, alitoa wito kwa wazazi na walezi kuwalea watoto katika njia ya kupenda mazingira ikiwamo suala la upandaji miti sehemu wanazoishi.

Alisema katika Ilani ya CCM ahadi ya 235 inaeleza namna ya mikakati ya kuhakikisha mazingira yanatunzwa sambamba na upandaji wa miti na ndiyo maana hata katika ziara zao wanahamasisha kila balozi wa nyumba kupanda miti angalau mitatu katika eneo lake analoishi.

"Niwe muwazi katika eneo hili wamekuwa wavivu kupanda miti kwani hata nyumba za walimu nazo hazina miti licha ya shule kuanzishwa tangu mwaka 1953, lakini pako jangwa niwaombe tupande miti tupende na tuitunze," alisema.

Katibu wa mpango wa upandaji miti Taasisi ya Habari Development Association, Bernard James, alisema Dodoma ndiyo makao makuu ya nchi hivyo ni lazima kuhakikisha wanapatengeneza na panakuwa pakijani na ndiyo fahari yetu.

Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde, alisema wamekuwa wakishirikiana kwa karibu na ofisi ya mkuu wa mkoa na wilaya katika jitihada za upandaji miti lengo likiwa ni kulifanya Jiji la Dodoma kuwa na mandhari nzuri.

"Tunataka jiji letu la Dodoma lifanane na majiji mengine duniani kuhakikisha tunaondokana na hali ya ukame na hatimaye mkoa unakuwa wa kijani," alisema Mavunde.

# COSTECH kuendeleza ubunifu wa vijana

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) imesema inaendeleza jitihada za kufanya uatamizi wa mawazo ya vijana na watu wenye teknolojia ya ubunifu ili kuwawezesha kuishi katika ndoto zao.

Ofisa uhusiano wa tume hiyo, Mary Kigosi, alibainisha hayo juzi jijini Dodoma, wakati akiongea na waandishi wa habari kwenye maonyesho ya ubunifu yaliyoandaliwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kushirikiana na Shirika la SIDA.

Kigosi, alisema watu wengi wamefanikiwa baada ya ufadhili wa taasisi hiyo inayowabeba kwenye utafiti, ubunifu na huduma na walengwa huwa ni vijana.

"Kuna vijana wengi wana ndoto kubwa, lakini hawana uwezo wa kuzifikia kutokana na kushindwa kugharamia, tunatumia nafasi hiyo kuwasaidia kutimiza ndoto zao," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya JV Biotech Enterprise Co Ltd, Jacob Tito ambaye ni mnufaika wa COSTECH, aliwashauri vijana wenye ujuzi kuona haja ya kutafuta fursa ili kuondokana na tatizo la ajira.

"Mimi ni muhitimu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na mmiliki kiwanda cha kusindika mazao ya muhogo baada ya kuwezeshwa mtaji na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknojia (COSTECH) naamini kuna vijana wenzangu wengi wabunifu, lakini wanashindwa namna ya kutimiza ndoto zao kutokana na kukosa mitaji," alisema.

Aliwashauri vijana kushirikiana na tume hiyo na wataona manufaa yake kwenye sekta za uchumi wa viwanda.

Vilevile, alisema kupitia kampuni hiyo wameajiri vijana watano ajira za kudumu na za muda vijana 25 hiyo ni kutoka na mkopo waliopatiwa na COSTECH wa Sh. milioni 40.

Kadhalika COSTECH ilifadhili mradi wa utafiti wa gugu vamizi katika Wilaya ya Kongwa lililokuwa linatishia uzalishaji wa malisho ya mifugo.

Notkery Mwalongo, mtafiti kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, alisema kutokana ufadhili walioupata kutoka COSTECH, wamefanikiwa kudhibiti gugu hilo vamizi ambalo lilikuwa linatishia uzalishaji wa malisho ya mifugo katika Ranchi ya Taifa ya Mifugo ya Kongwa.



Mbunge wa Bahi, Kenneth Nollo (kushoto), akimkabidhi msaada wa mifuko 60 ya saruji Mwenyekiti wa Kijiji cha Msisi Juu, Samson Mwangwela, kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye Shule ya Msisi iliyoko Wilaya ya Bahi mkoani Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Maambukizi VVU/UKIMWI yadhibitiwa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amesema kuwa serikali imepiga hatua kubwa katika kudhibiti maambukizi ya VVU na UKIMWI.

Amesema kiwango cha upimaji wa VVU kimeongezeka kutoka asilimia 61 hadi 83 ya makisio ya watu wanaoishi na VVU (WAVIU).

Mhagama alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani yatakayofanyika Desemba mosi.

Alisema kiwango cha upimaji wa VVU kimeongezeka kutoka asilima 61 ya makisio ya watu wanaoishi na VVU (WAVIU) mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 83 mwaka 2019 na serikali kupitia uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan imepiga hatua kubwa katika kudhibiti.

Alifafanua kuwa matumizi ya dawa za kufubaza VVU (ARV) kwa WAVIU wanaojua hali zao za maambukizi yameongezeka kutoka asilimia 95 mwaka 2016 hadi asilimia 98 mwaka 2019 na kiwango cha kufubaza VVU kwa wale wanaotumia ARV kimeongezeka kutoka asilimia 87 mwaka 2016 hadi asilimia 92 mwaka 2019.

Pia alisema vifo vitokanavyo na Ukimwi vimepungua kwa asilimia 50 kutoka vifo 64,000 mwaka 2010 hadi 32,000 mwaka 2020, wakati takwimu za kiwango cha maambukizi katika jamii (HIV prevalence) zinaonyesha kilishuka kutoka asilimia saba mwaka 2003/2004 hadi 4.7 mwaka 2016/17.

Alifafanua kuwa maambukizi mapya ya VVU kwa watu wazima nchini Tanzania yameshuka kutoka 110,000 mwaka 2010 hadi 68,000 mwaka 2020.

"Wakati maambukizi mapya kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto (Mother to child transmission) yameshuka kutoka asilimia 18 mwaka 2010 hadi asilimia saba mwaka 2020."

Akizungumza kuhusu maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani kwa mwaka huu alisema yanatarajiwa kufanyika kitaifa jijini Mbeya kuanzia Novemba 24 hadi Desemba 1, katika Uwanja wa Luanda Nzovwe na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Aliongeza kuwa lengo la maadhimisho ya siku hiyo ni kutoa fursa ya kutathmini hali halisi na mwelekeo wa kudhibiti virusi vya UKIMWI (VVU) kitaifa na kimataifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS), Dk. Leonard Maboko, aliishukuru serikali kwa kuendelea kupambana na maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI ili kuhakikisha jamii inakuwa salama na kuendelea kushiriki katika shughuli za uzalishaji.

Mwenyekiti wa Baaza la Taifa la Watu Wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (NACOPHA), Leticia Kapela, aliipongeza serikali kwa kuwajali watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na mikakati iliyojiwekea katika mapambano hayo ambayo yameleta mafanikio kupunguza maambukizi.





# Watumia punda kusafirisha wagonjwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKAZI wa Kijiji cha Kilambo kilichoko Kata ya Mwatenga, Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, wamesema hulazimika kutumia punda kuwasafirisha wagonjwa kwenda hospitalini nyakati za masika kutokana na mawasiliano ya barabara kukatika.

Wakizungumza na Nipashe, wananchi hao walisema barabara yao ambayo haijawahi kujengwa tangu nchi ipate uhuru, imechimbika na kuwa korongo linalojaa maji na kusababisha isipitike kirahisi kwa chombo chochote cha usafiri.

Walisema hali hiyo husababisha wanafunzi hasa wale wa shule za msingi walio katika madarasa ya chini kulazimika kusitisha masomo kwa kuhofia kusombwa na maji yanayotiririka kwenye barabara hiyo.

Mmoja wa wananchi wa kijiji hicho, Tatizo Jamson, alisema, kipindi cha masika, usafiri pekee unaoweza kutumika kupeleka wagonjwa hospitalini ni punda ambao huwabeba hadi kwenye zahanati ya kijiji na ikionekana wanatakiwa kwenda Hospitali ya Misheni ya Chimara hubebwa na matrekta madogo maarufu kama Power Tilla.

"Barabara yetu haijawahi kulimwa na greda tangu nchi yetu ipate uhuru, kila mwaka inachimbika na sasa imekuwa korongo kubwa linalopitisha maji mengi wakati wa masika na kusababisha mawasiliano ya barabara kukatika," alisema Jamson.

Jamson aliiomba serikali kuiangalia barabara hiyo na kuwasaidia japo kuinua tuta ambalo watalitumia kupita wakati wa msimu wa mvua unapofika.

Bibi Jamila Masoud (62), alisema kuwa mwaka jana aliugua na kubebwa kwa punda kupelekwa zahanati na nusura apoteze maisha baada ya kuzimia na kurejeshwa nyumbani wakidhani tayari amekufa.

"Mwaka jana niliugua wakanibeba kwenye punda kwenda hospitali, njia ilikuwa imejaa maji, nikafia (kuzimia) kwenye musisi (mti wa Ukwaju) pale, wakaibeba maiti yangu kuirudisha nyumbani, lakini kwa bahati nzuri nikapigwa upepo nikaamka," alisema bibi Jamila.

Alisema barabara hiyo imekuwa ikiwatesa kwa muda mrefu na kuiomba serikali iwasaidie kuijenga ili kuwaondolea adha zinazowakumba hasa kipindi cha masika.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Kilambo, David Shanjila, alisema wakati wa msimu wa mvua, shule yao huwa na mahudhurio hafifu kutokana na wanafunzi wengi kushindwa kwenda wakihofia kusombwa na mafuriko ambayo yanapita kwenye barabara.

Alisema hali hiyo husababisha kazi yao kuwa ngumu kwa sababu hata idadi ndogo ya wanafunzi wanaofika shuleni hufika kwa kuchelewa na baadhi yao sare zao na madaftari yanalowana na kushindwa kuandika chochote.

Alisema tatizo hilo linaathiri ufaulu wa wanafunzi wa shule hiyo na kwamba endapo haitatengenezwa vizuri kuna hatari wanafunzi wa eneo hilo kuendelea kutofanya vizuri.

"Baadhi ya wanafunzi huwa wanasombwa na maji, bahati nzuri wanaokolewa na watu wazima, ikitokea hivyo hawa wanafunzi kesho yake huwezi ukawaona tena," alisema Mwalimu Shanjila.

Baadhi ya wanafunzi wa shule hiyo walisema wakati wa masika wanalazimika kutokwenda shule kwa sababu barabara inajaa maji na hata wakienda wanafika mchana muda ambao hawawezi kusoma vizuri.

Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, alikiri ofisi yake kupokea malalamiko ya wananchi hao na kwamba serikali ipo kwenye mipango ya kuijenga kwa kiwango ambacho kitawasaidia kutembea na kufanya shughuli zao bila vikwazo.

"Serikali imetenga Sh. milioni 210 kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha changarawe, mkataba ulisainiwa Oktoba 18, mwaka huu kati ya TARURA na mkandarasi na kazi inaanza kufanyika hivi karibuni," alisema Mfune.

Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA), Wilaya ya Mbarali, Mhandisi Abdul Mfundili, alisema barabara hiyo ina urefu wa kilomita 18.6 na yote itajengwa pamoja na makaravati sita ili kupunguza maji.

Vilevile, alisema watainua tuta ili kuzuia maji yasiingie barabarani na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara hiyo ambayo ni muhimu kwa wakazi wa kijiji hicho.



Baadhi ya wajasiriamali wa Jiji la Mbeya wakiendelea kufanya biashara katika kituo cha daladala cha Kabwe mwishoni mwa wiki, eneo ambalo walizuiliwa na serikali kutokana na kutengwa kwa ajili ya daladala. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Chunya watakiwa kujiandaa mabadiliko tabianchi

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI wa Wilaya ya Chunya, mkoani Mbeya wametakiwa kujiandaa na mabadiliko ya tabianchi hasa uhaba wa mvua uliotangazwa na Mamlaka ya Hali ya Hewa nchini (TMA) kuyakumba baadhi ya maeneo nchini.

Ofisa Kilimo wa Wilaya hiyo, Cuthbert Mwinuka, alitoa tahadhari hiyo juzi alipokuwa anazungumza na wananchi wa Kijiji cha Igangwe, Kata ya Lualaje na kuwataka kuhakikisha wanapanda mazao yanayokomaa kwa muda mfupi.

Aliwataka pia kupanda mazao yanayohimili ukame ikiwamo mihogo, viazi na alizeti huku akiwataka wafugaji wenye mifugo mingi kuipunguza ili wasiingie hasara kwa madai kuwa hali hiyo itasababisha mifugo kukosa chakula na kufa.

Mwinuka alisema kwa maelezo ya TMA, mwaka huu kutakuwa na tatizo kubwa la uhaba wa mvua na katika wilaya hiyo kuna maeneo ambayo mvua itakuwa chini ya wastani na kutaka kuwa wajihami.

"Kwa mtu yeyote mwenye nguvu za kufanya kazi hakikisheni mnalima angalau kuanzia ekari mbili za mihogo, viazi na alizeti, kwa wakulima wa mahindi jitahidi kupanda mbegu zinazochukua muda mfupi kukomaa," alisema Mwinuka.

Alisema kwa sasa zipo mbegu za mahindi ambazo zinakomaa baada ya siku 75 na kwamba hizo ndizo wakulima wanashauriwa kuzilima ili ziendane na kiwango cha mvua kilichopo.

Baadhi ya wakulima wa eneo hilo waliiomba serikali kuwasaidia wapate pembejeo za kilimo mapema ili waendane na msimu wa mvua na wazalishe kiasi cha mazao kinachohitajika kwa ajili ya chakula na biashara.

Mmoja wa wakulima hao, Joel Mtinda, alisema katika eneo lao wamekuwa wakipata pembejeo kupitia Chama Kikuu cha Wakulima wa Tumbaku wilayani humo (CHUTCU), lakini safari hii mpaka sasa hawajapata.

Alisema hali hiyo inawapa wasiwasi kwamba watashindwa kuendana na msimu kama ilivyoshauriwa na serikali na kuomba serikali iwasaidie kabla mvua haijaanza kunyesha.

"Barabara zetu mvua ikianza kunyesha huwa hazipitiki kirahisi na hivyo kusababisha hata bei za pembejeo kupanda kuliko kawaida, sasa ili tuendane na msimu kama serikali inavyotushauri ni vizuri itusaidie tupate pembejeo hizi mapema," alisema Mtinda.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliuagiza uongozi wa CHUTCU kusimamia na kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo kabla mvua haijaanza kunyesha ili wasije wakakwama kupanda mazao yao na wakashindwa kuendana na msimu.

Aliuagiza uongozi wa chama hicho kikuu kuhakikisha ndani ya wiki mbili wakulima wanapata mbolea na kuhakikisha mgawo unakuwa sio wa upendeleo kulingana na maeneo.

"Mbolea hiyo mnawapatia wakulima kwa njia ya mkopo na mnawakata kwenye mauzo ya tumbaku tena kwa viwango vya dola, sasa nawapa wiki mbili nipate taarifa kwamba mmeshawapatia mbolea, na hayo magari mnayosema yapo njiani yanakuja nataka nipate taarifa ya uhakika," alisema Homera.

## CWT yaiomba serikali kulipa madai ya walimu kwa wakati

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT) Wilaya ya Mbeya kimeiomba serikali kulipa kwa wakati madai ya wanachama wake ambayo hayahusiani na mishahara yanayolimbikizwa katika ngazi ya halmashauri ili kuongeza ari na ufanisi wa kazi.

Alitoa ombi hilo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano mkuu wa kawaida wa chama hicho ngazi ya wilaya ambacho kilikuwa na lengo la kujengeana uwezo na kwamba malimbikizo ya madeni hayo huwa yanawakatisha tamaa walimu.

Katibu wa CWT Wilaya ya Mbeya, Mwalimu Sekela Simon, alisema wakati mwingine mwalimu anaweza akahamishwa na serikali kutoka kituo kimoja cha kazi kwenda kingine bila kulipwa stahiki zake kwa muda mrefu.

Alisema baadhi ya madeni hayo huwa yanadumu kwa zaidi ya mwaka mmoja hali ambayo inawafanya walimu kuwa na manung'uniko na kushindwa kufanya kazi kwa moyo.

"Haya madeni yasiyohusiana na mishahara huwa yanatengenezwa na halmashauri, sasa tunaiomba serikali ijitahidi kulipa madeni hayo kwa wakati ili walimu tufanye kazi kwa moyo," alisema Mwalimu Sekela.

Mwenyekiti wa CWT Wilaya ya Mbeya, Anthony Mwaselela, alisema katika kikao walichokifanya walikubaliana kuwa ifikapo Februari mwakani, madeni yote ya walimu yawe yamelipwa ili waendelee kufanya kazi kwa moyo.

Alisema baadhi ya madeni hayo yanatokana na likizo za walimu, wastaafu kurejeshwa majumbani pamoja na uhamisho wa walimu kutoka kituo kimoja kwenda kingine.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Steven Katemba, alisema wanakusudia kuanza kulipa madeni hayo kwa awamu ili mpaka kufikia mwezi Februari baadhi ya madeni hayo yawe yameshalipwa.

Alisema wataanza na madeni yanayohusiana na likizo za walimu na kwamba watakaa na viongozi wa CWT ili wakubaliane madeni yatakayofuata na yatakayomaliziwa.

# Wabaini kiini mimba za utotoni

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

ASILIMIA 12 ya watoto wenye umri wa kuanzia miaka 10 hadi 15 Zanzibar wanashiriki tendo la kujamiiana, hali inayosababisha kupata madhara mbalimbali ikiwamo mimba za umri mdogo.

Mratibu wa mradi wa 'O3 Our Rights, Our Lives, Our Future', Hasina Bukheti, alibainisha hayo wakati wa warsha ya kuwajengea uwezo maofisa takwimu wa Wizara ya Elimu kuhusu mwitikio na upimaji wa viashiria vya kimataifa vya elimu ya UKIMWI, afya ya uzazi na stadi za maisha kwa wanafunzi shuleni.

Warsha hiyo iliandaliwa na Shirika la Kimataifa la Elimu na Sayansi (UNESCO) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Sweden (SIDA).

Alisema takwimu hizo ni kwa mujibu wa utafiti uliofanya na Tume ya Ukimwi Zanzibar mwaka 2016 uliobaini bado kuna hali mbaya kwa watoto kujiingiza katika uhusiano wa kimapenzi wakiwa na umri mdogo.

Alisema kuwa kwa mujibu wa utafiti uliofanywa mwaka 2016 na nchi za kusini mwa jangwa la sahara, asilimia 28 ya wasichana wamejifungua wakiwa na umri wa miaka 18 na asilimia 12 huolewa.

"Kwa mujibu wa utafiti huo kati ya asilimia tano na asilimia 25 ya wasichana waliobalehe, wameshajamiiana wakiwa chini ya umri wa miaka 15," alibainisha.

Mratibu huyo alisema utafiti huo pia umebainisha kuwa maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi yamefikia 141,000 kwa wanaume na 290,000 kwa wanawake wenye umri wa miaka 15 hadi 24.

Akitoa mada kuhusu elimu ya afya ya uzazi, Ukimwi na stadi za maisha, Ofisa Ukimwi, Afya ya Uzazi na Dawa za Kulevya kutoka Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha, Riziki Mohammed Juma, alisema kutokana na mabadiliko ya tabia za watu, kuna haja elimu ya afya ya uzazi kutolewa kwa watoto kuanzia ngazi ya elimu ya maandalizi ili kulinda viungo vyao vya uzazi.

Alisema elimu hiyo itamsaidia mtoto kumlinda na vitendo vya udhalilishaji kwa sababu wengi wao hawajui athari ya vitendo hivyo.

Aliwataka walimu kuwafundisha watoto kufanya usafi wa mwili ikiwamo katika sehemu za siri ili kuepukana na bakteria mbalimbali ambao wanasababisha kuharibu afya ya uzazi.

Kwa washiriki wa mafunzo, walisema kuwa watahakikisha mafunzo waliyopatiwa wanayafanyia kazi ili kukusanya takwimu zinazohitajika ikiwamo za udhalilishaji kwa wanafunzi.



Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Msoud Othman (katikati), akikata utepe kuashiria uzinduzi rasmi wa kampeni maalum ya chanjo dhidi ya Uviko-19 uliofanyika Viwanja vya Kisonge Michenzani mjini Zanzibar. Kampeni hiyo inakwenda sambamba na maadhimisho ya Siku ya Kisukari Duniani. Kushoto ni Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makamu wa Rais ahimiza wananchi chanjo corona

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema wagonjwa wa kisukari wanaathirika zaidi na ugonjwa wa Uviko-19, hivyo amewahimiza wananchi kuchanja chanjo ya corona.

Othman aliyasema hayo mjini Zanzibar katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kisukari Duniani, iliyokwenda sambamba na uzinduzi wa kampeni maalum ya siku 12 ya chanjo dhidi ya Uviko-19 iliyoanza juzi kwa wilaya zote Unguja na Pemba.

Alisema maradhi ya kisukari hivi sasa yameingiwa na janga la maradhi ya Uviko-19 na hivyo kuchangia kuwapo athari kubwa zaidi kwa wagonjwa wa kisukari ambao wanaathirika kwa wepesi zaidi wakipata ugonjwa wa corona na kuwahimiza wananchi wote kuchanja.

Alisema kiwango cha tatizo la maradhi ya kisukari kimeongezeka sehemu mbalimbali duniani na Zanzibar ongezeko hilo ni la kasi kubwa na linawaathiri hata watoto wadogo huku watu maskini wakiwa waathirika zaidi wa maradhi hayo.

Alisema mwanzo ugonjwa wa kisukari ulipoingia, ulikuwa unawapata watu wenye uwezo wa kipato lakini hivi sasa hali imebadilika kwa maana hauchagui.

Othman aliitaka jamii kupunguza utamaduni wa kula vyakula vyenye mafuta mengi, wanga na sukari kwa wingi ili kuondosha uwezekano wa kupata kisukari kwa kuwa vyakula hivyo ndio chimbuko kubwa la kupata maradhi ya kisukari.

Alisema kumekuwa na tatizo kwa watoto hasa shuleni kujengewa utamaduni wa kula vyakula ambavyo ni chanzo kikuu cha tatizo la kisukari na kwamba kuna haja pia mamlaka zinazosimamia ubora wa vyakula kuangalia udhibiti na ubora wa vyakula wanavyokula watoto katika shule mbalimbali nchini ili kudhibiti ugonjwa wa kisukari usiwaathiri watoto.

Alisema kuna haja jamii kuangalia na kuzingatia matumizi ya lishe sahihi katika vyakula mbalimbali wanavyokula ikiwa ni pamoja na kujenga uwelewa wa lishe bora ili kuepuka uwezekano wa kupata maradhi hayo.

Othman alipongeza kuwapo mwamko mkubwa wa jamii kufanya mazoezi ikiwa ni sehemu ya jitihada za pamoja za kupambana na maradhi ya kisukari na kuwataka wananchi kuendelea na utamaduni wa kufanya mazoezi kupambana na kisukari.

Alishauri kampeni ya kisukari Zanzibar iwe ya kitaifa na ifanyike kuanzia ngazi ya shehia, wilaya, mikoa hadi taifa kwa kuwa kisukari sasa ni janga la taifa na kwamba jambo hilo litasaidia mwamko zaidi kwa jamii.

Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, alisema mgonjwa mwenye kisukari anaweza kuathirika zaidi iwapo atapata corona.

Alisema Zanzibar ina dozi za kutosha za chanjo ya corona, hivyo aliwahimiza wananchi kupata chanjo hiyo ili kudhibiti maambukizi.

Mazrui alisema magonjwa yasiyoambukiza yanaathiri jamii na kupunguza nguvu kazi za kiuchumi na serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa kupambana na maradhi hayo ikiwa ni pamoja na kutoa tiba kupunguza athari zaidi zitokanano na ugonjwa huo.

## Waziri ataka kampeni bidhaa za Zanzibar

Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga, amesema kuna haja kuanzishwa kampeni maalum ya kushajihisha bidhaa zinazozalishwa Zanzibar ili kujenga imani ya uzalishaji wa bidhaa ndani na nje ya Zanzibar.

Soraga aliyasema hayo jana huko Maruhubi nje ya Mji wa Zanzibar wakati akizindua ushirika wa viwanda.

Alitolea mfano wa nchi ya Afrika Kusini ambayo inatangaza bidhaa zao, hivyo ni vyema Zanzibar kuwa na kampeni hiyo hasa ikizingatiwa kuwa Zanzibar ina uwezo wa kuzalisha bidhaa za viwanda ambazo zina ubora wa kitaifa na kimataifa.

Alisema lazima kuwa mfano wa kusimamia mnyororo wa thamani wa bidhaa za viwanda na kuwa mwamvuli wa kufanikisha jukumu hilo.

Alisema serikali inathamini mchango wa sekta ya uzalishaji na itaendelea kuchukua kila juhudi za kuvilinda viwanda vya ndani na kuondokana na Zanzibar inaagiza kila kitu kutoka nje wakati ina uwezo wa kuzalisha baadhi ya bidhaa zinazoagizwa.

Waziri huyo alisema endapo ikifanikiwa, serikali itafanya udhibiti wa uingizaji wa bidhaa zinazoingia Zanzibar licha ya kuwapo dosari kwa wafanyabiashara ambao baadhi yao huingiza bidhaa zisizo na ubora.

Mwenyekiti wa Kampuni ya Ushirika wa Viwanda Zanzibar, Balozi Amina Salum Ali, alisema lengo la ushirika ni kuwawezesha wajasiriamali wanawake kutengeneza bidhaa zenye kiwango na kuuza ndani na nje ya nchi.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Sekta ya Viwanda, Dk. Abdallah Rashid, alisema kuwa hadi kufikia mwaka 2012, sekta ya viwanda imeajiri wananchi 10,427 na hadi kufikia mwaka 2019 kulikuwa na ongezeko la ajira 1,174.

Alisema hali hiyo imesababisha sekta ya viwanda kukua kwa asilimia 10.6 ambapo kilimo kilikua kwa asilimia 2.6 na huduma asilimia 8.7.

Alisema kwa mwaka 2017, sekta ya huduma ilichangia asilimia 48.6, mwaka 2018 asilimia 51.3 na mwaka 2019 asilimia 50.6 na kwa upande wa sekta ya viwanda kwa mwaka 2017 ilichangia asilimia 19.6, mwaka 2018 asilimia 17.8 na mwaka 2019 asilimia 18.3.

Alisema taifa lililowekeza kwenye viwanda linakuwa na uchumi imara na endelevu na kuhimili majanga mbalimbali ambayo huikumba dunia, lakini uzalishaji wa bidhaa za viwanda unachochea biashara mbalimbali katika nchi na kuongeza ajira nyingi.

Mkurugenzi wa Ushirika wa Viwanda Zanzibar, Dk. Sira Ubwa Mamboya, alisema wazalishaji na wajasiriamali wadogo wanaongoza katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kwa matumizi ya Zanzibar na sekta ya ujasiriamali imeongeza ajira kwa vijana.

Alisema ushirika wa viwanda una jukumu la kuwakusanya pamoja na kuwasimamia vijana na wanawake wazalishaji na wajasiriamali ili kutumika katika uzalishaji kwenye sekta zote ikiwamo kilimo, uvuvi, viwanda na kazi zingine za mikono.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**ABDULMAJIDI RAMADHANI SAID** anatangaza kupotelewa na result slip ya kidato cha sita yenye index namba S1129/0543 iliyotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **IGUGUNO** mwaka 2021,yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **DAR/CHU/RB/542045/2021**

## KUPOTEA KWA KADI ZA MAGARI

ROGERS SABDIEL MZIRAY Anatangaza kupotelewa na kadi za magari zenye namba za usajili T994 AAJ, T300 AEL, T626 ARQ. Kwa yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi kwa namba ARU/KIK/RB/539230/2021.

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**
**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMB.NA. MG/LD/8276/7**
**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: ANTHONY L. KIWAMBO S.L.P 406, MOROGORO.**
**ARDHI: KIWANJA NA 363 KITALU ''EE''AREA 6 MANISPAA YA MOROGORO**
**MUOMBAJI: AGNES ALPHONCE MAKIVYA S.L.P 406, MOROGORO.**

Taarifa inatolewa kwamba **BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalo tolewa kwa muda wa mwezi mmoja toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti.
**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana, irudishwe kwa **MKURUGENZI WA MANISPAA-MOROGORO S.L.P 166 MOROGORO**

Valency HK
**KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO**

ROYAL RUNNER'S AND GENERAL SUPPIES T.LTD & COURT BROKER

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

TUTAFANYA MNADA TAREHE 30/11/2021 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA NYUMBA ILIYOPO MTAA WA VINGHAWE MPWAPWA MJINI MALI YA AIDANI MLAKU BAADA YA KUSHINDWA KESI JINAI NO. 86/2020 YA JOHN ABINEL LUBELEJE. MNADA UTAFANYIKA MAHALI NYUMBA ILIPO.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0756900540/ 0713913150.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ROSE AGGREY TEEMBA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 853 ANG – MITSUBISH FUSO.** Chassis namba **FK417E550495.** Engine namba **6D16716177.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/GOG/RB/542724/2021.**

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION**
**CAUSE NO 38 OF 2021**
**In the Matter of the Estate of the Late JOSEPH MVALO PEMBE**

**BY 1. APRONIA PASCHAL NICOLAUS**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above – named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 10 day of 11....2021

**Dated at Morogoro this 4 day of 11.....2021**

..................................
**RESIDENT MAGISTRATE**
RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O Box 660, Morogoro

116571402

***Uza,***
***Chenye Thamani***
***Kubwa Kwa***
***Kutangaza Nasi***
***Kwa Bei Poa***
***Tupigie***
***0782253676***

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Mwili wa De Klerk kuchomwa, mazishi faragha

**Johannesburg,** AFRIKA KUSINI

RAIS wa mwisho mzungu wa Afrika Kusini, FW de Klerk, aliyefariki akiwa na umri wa miaka 85 wiki iliyopita, atazikwa katika sherehe ya faragha siku ya Jumapili, kulingana na wakfu wake.

"Wakfu wa FW de Klerk unawatangazia kuwa kuchomwa kwa FW de Klerk' na mazishi yake yatafanyika Jumapili Novemba, 21," ilisema taarifa.

"Itakuwa sherehe ya faragha kwa familia na haitakuwa wazi kwa vyombo vya habari," Wakfu huo uliongeza. Hakuna maelezo zaidi yaliyotolewa.

De Klerk aliingia madarakani mwaka 1989 chini ya utawala wa ubaguzi wa rangi, mfumo ambao ulihalalisha ubaguzi wa rangi, baadaye akawa mtu muhimu katika kipindi cha mpito kuelekea demokrasia.

Mwaka 1993, alipata Tuzo ya Amani ya Nobel na Rais wa zamani Nelson Mandela kwa kusaidia kujadili kukomesha ubaguzi wa rangi.

Kumekuwa na hisia mseto kuhusu utawala wake Afrika Kusini. Alifariki Alhamisi, baada ya kupatikana na saratani mapema mwaka huu. **BBC**

# Watoto 45,000 kizuizini waachiliwa huru

**New York,** MAREKANI

UCHAMBUZI mpya uliotolewa na Shirika la Umoja wa Mataifa lakuhudumia watoto- (UNICEF), umeeleza, zaidi ya watoto 45,000 wameachiliwa huru kutoka kizuizini na kurudishwa kwa familia zao wakiwa salama au kutafutiwa njia mbadala inayofaa kwa malezi ya watoto tangu kuanza kwa janga la COVID-19.

Taarifa iliyotolewa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa UNICEF, Henrietta Fore kutoka jijini New York Marekani, ikiwa ni kuelekea kwenye kongamano la dunia la haki za watoto iliongeza kwamba, uchambuzi huo ni ushahidi tosha suluhisho ya haki rafiki kwa watoto.

"Tumejua kwa muda mrefu kwamba mifumo ya haki haina vifaa vya kushughulikia mahitaji maalum ya watoto, hali ambayo inazidishwa na janga la COVID-19. Hata hivyo tunapongeza nchi ambazo zilitii wito wetu na kuwaachilia watoto kutoka kizuizini.

Kwa kuwalinda watoto kutokana na hali ambazo zingeweza kuwaweka hatarini zaidi kwa ugonjwa mbaya, nchi hizi ziliweza kushinda upinzani wa umma na kuchochea masuluhisho ya haki yanayolingana na umri," alisema Fore. **UN**

# Wanajeshi wahukumiwa kifo mauaji raia Uganda

**Kampala,** UGANDA

MAHAKAMA ya Jeshi Uganda, imetoa adhabu ya kifo kwa wanajeshi wawili waliohusika katika mauaji ya raia nchini Somalia, Agosti mwaka huu.

Wenzao watatu wamehukumiwa kifungo cha miaka 39 gerezani kwa kuhusika katika maovu hayo ambayo yalizua ghadhabu nchini Somalia.

Nchini Somalia, habari za hukumu hiyo imewaridhisha jamaa za waliouawa.

**Wanajeshi wa Uganda ni sehemu ya vikosi vya AMISOM vinavyolinda amani nchini Somalia.**

Wanajeshi wa Uganda ni sehemu ya vikosi vya AMISOM vinavyolinda amani nchini Somalia.

Kulingana na kanuni za majeshi ya walinda amani Somalia AMISOM, mwanajeshi yeyote anayetenda mauaji kinyume na shughuli za kulinda amani anatakiwa kupata adhabu kali.

Mahakama ya Jeshi ya Uganda, ilisikiliza ushahidi wa eneo kulikotokea mauaji hayo, hii ikiwa ndiyo mojawapo ya njia za kudhihirisha uwazi na uwajibikaji kwa raia wa Somalia.

Wakuu wa AMISOM nchini Somalia pamoja na katika serikali wameridhia mchakato wa Uganda katika kuendesha kesi hiyo. Uganda ilikuwa taifa la kwanza kupeleka majeshi Somalia mwaka 2007 na kumekuwapo na hukumu kadhaa zinazotolewa kwa wanajeshi watovu wa nidhamu. **DW**



Balozi aliyekuwa akiiwakilisha Marekani kwenye Umoja wa Mataifa, Bill Richardson, kulia, akiwa pamoja na mwandishi wa habari Danny Fenster, jijini Naypyitaw, nchini Myanmar, jana. Mwandishi huyo raia wa Marekani, ameachiwa huru kutoka jela, siku chache baada ya kuhukumiwa miaka 11 na kufanya kazi ngumu nchini Myanmar. **PICHA: AP**

# Watu 20 wauawa kwenye shambulio

**Ouagadougou,** BURINA FASO

WATU 20 wameuawa, wakiwamo wanajeshi 19 na raia mmoja katika Jimbo la Soum, nchini Burkina Faso. Shambulio hilo lilitokea Jumapili hii, Novemba 14.

Watu wenye silaha walivamia kikosi cha wanajeshi mapema asubuhi Jumapili, Novemba 14. Ni moja ya mashambulizi mabaya zaidi kutekelezwa dhidi ya vikosi vya ulinzi na usalama tangu mashambulizi hayo kuanza nchini humo.

"Takwimu ambazo mara nyingi ni vigumu kukubalika tunapokuwa na waathiriwa tangu tumekuwa katika hali hii ya vita" alitangaza Ousséni Tamboura, msemaji wa serikali, akitangaza habari za shambulio hilo.

Shambulio ambalo lilitokea kwenye mgodi wa zamani wa Inata. Watu wenye silaha waliokuja kwa pikipiki na magari madogo, kulingana na vyanzo vya usalama, walishambulia kikosi cha wanajeshi mwendo wa saa 11 alfajiri. Na kulikuwa na mapigano.

"Tulikabiliwa na shambulio la kinyama, lakini wanajeshi wetu walionyesha ujasiri na upinzani mkubwa dhidi ya adui," alisema Maxime Koné, Waziri wa Usalama.

Jeshi la Anga, liliitwa kusaidia kurejesha udhibiti wa eneo lililoshambuliwa. Chanzo cha usalama kilisema watu waliotekeleza shambulizi hilo walikuwa hapo kuanzia saa tisa usiku na walikaa hapo hadi 12 asubuhi. Operesheni ya kutafuta watu wanaosadikiwa kutoweka inaendelea.

Eneo ambalo shambulio hilo lilifanyika ni kubwa kabisa kwa mujibu wa mamlaka.

Ijumaa, Novemba 12, maofisa saba wa polisi, waliuawa katika shambulio katika eneo hilo. **RFI**

# PAULSEN AZITAKA CAF, FIFA KUIADHIBU MADAGASCAR

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Madagascar, Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Kim Poulsen, ameonyesha kukerwa na mambo yasiyo ya kiungwana waliyofanyiwa viongozi na wachezaji wa timu hiyo baada ya kuwasili nchini humo na anaamini kuwa Shirikisho la Soka Duniani (FIFA) na la Afrika (CAF), hayatosita kuchukua hatua.

Juzi, kwenye Uwanja wa Mahamasina jijini Antananarivo nchini Madagascar, Stars ilicheza mechi hiyo bila nahodha wake Mbwana Samatta, kipa namba moja Aishi Manula na beki wa kati, Bakari Mwamnyeto, baada ya kudaiwa kuwa walikuwa na maambukizo ya virusi vya corona, kitu ambacho kilipingwa na maofisa wa Shirikisho la Soka nchini (TFF) kwa maelezo kuwa wachezaji wote walipimwa nchini kabla ya kuondoka na wote walikuwa hawana maambukizo hayo.

"FIFA na CAF wanaelekeza maendeleo ya soka na kucheza kiungwana na Watanzania ni wakarimu, wana msemo wao wa 'karibu' kwa watu na wageni wanaokuja, hali inayowafanya kuwa na amani na furaha wanapofika kwao, hata Madagascar walikaribishwa hivyo.

"Sisi kwao hawakuwa waungwana kwa sababu hawakufungulia mlango wa ndege kwa dakika 75 na walijaribu kutubughudhi kwa kila njia," alisema Paulsen.

Akionyesha kukerwa zaidi na hali hiyo, kocha huyo alionekana kuelezea zaidi figisu kuliko hata jinsi mpira ulivyochezwa uwanja, alisema wachezaji wote wa Stars walipimwa nchini Tanzania kabla ya kuondoka na hawakukutwa na ugonjwa wowote, lakini anashangaa kuona hali ilibadilika.

'Nafikiri FIFA na CAF watachukua hatua, hii ni lazima waadhibiwe, mpira wa Afrika uachwe uchezwe kiungwana ndani na nje ya uwanja, tumepata sare kwenye mechi hiyo, tumeipata ugenini tena baada ya kutuzuia wachezaji wetu muhimu," alisema.

Poulsen alieleza kushangazwa na figisu hizo wakati Madagascar haikuwa na nafasi yoyote ile ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo ya kusaka tiketi ya kucheza Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar.

Stars imemaliza ikiwa kwenye nafasi ya tatu kwa pointi nane, Madagascar ikishika mkia kwa alama nne, DR Congo ikiwa kinara wa Kundi J kwa pointi 11, baada ya juzi kuifunga Benin mabao 2-0 na kuiacha na alama zake 10, hivyo kutinga hatua ya mtoano.

KIVUMBI...



Wachezaji wa Timu ya Fedha FC, Mwinyi Jumapili (kushoto) na Sadik Adam, wakiwania mpira wakati wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Hospitali ya Kivule jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Maisha Magic Bongo kufunga mwaka na tamthilia kali mpya

**Na Mwandishi Wetu**

MOTO wa burudani ndani ya Chaneli maarufu ya Maisha Magic Bongo (MMB), unashika kasi baada ya kutangaza kuzindua tamthilia mpya mbili kwa mpigo na kuifanya chaneli hiyo kuendelea kuwa kinara wa tamthilia na filamu za Kitanzania ndani na nje ya nchi.

Wapenzi wa filamu wamepewa zawadi ya aina yake ya kumalizia mwaka kwani tamthilia hizo mbili - La Familia na Danga zimeanza kurindima kuanzia jana katika Chaneli ya MMB - DStv 160.

Akizungumza na mwandishi wetu jana kuhusu tamthilia hizo, Mkuu wa Chaneli ya MMB, Barbara Kambogi, alisema wakati wote chaneli hiyo imehakikisha kuwa inatoa fursa kwa tasnia ya filamu hapa nchini kwa kuchukua filamu nyingi kutoka Tanzania ambapo kwa sasa zaidi ya asilimia 90 ya maudhui yao ni ya Kitanzania.

"Tamthilia hizi mbili zimezalishwa na wazalishaji wa kitanzania na kuigizwa na Watanzania katika mazingira yetu ya Kitanzania. Hizi ni tamthilia za Kitanzania kwa asilimia 100," alisema Barbara.

Msimu huu Maisha Magic Bongo inazindua tamthilia mpya pamoja na wazalishaji wapya ikionyesha ni kiasi gani imejikita katika kukuza vipaji vya Watanzania wenye udhubutu wa kushiriki katika sanaa.

Kuhusu Danga, ni tamthilia iliyotengenezwa na kijana maarufu, Idris Sultan aliyejipatia umaarufu wake kupitia kipindi cha Big Brother Africa kinachoandaliwa na MultiChoice Africa.

"Tunajivunia kufanya kazi na msanii aliyekuwa kupitia uwanja wetu na tunaamini kazi aliyoifanya kwenye Danga itapokelewa vizuri na watazamaji wetu. Tamthilia hii inataanza kuruka rasmi Jumatatu (jana) kuanzia saa moja na nusu usiku ndani ya Maisha Magic Bongo kila Jumatatu hadi Jumatano kila wiki," alisema Barbara.

Kwa upande wa tamthilia ya La Familia, Barbara alisema ni tamthilia yenye visa na vimbwanga vingi ndani ya familia ikiwa imebeba uhalisia wa familia za Kitanzania kwa ujumla.

"Mtengenezaji wa tamthilia hii ni Maximillian Rioba ambaye ni ingizo jipya la watengenezaji filamu ndani ya Maisha Magic Bongo. Tamthilia ya La Familia itaanza rasmi Jumatatu (jana) na itakuwa ikiruka Jumatatu hadi Ijumaa kuanzia saa nne usiku," alisema.

Aidha, aliwataka watazamaji wa chaneli hiyo kuendelea kuangalia vipindi vingine vingi zaidi ndani ya Maisha Magic Bongo kama ikiwamo Juakali; Jumatano hadi Ijumaa saa 3:30 usiku, Kitimtim; Jumatatu hadi Jumanne saa 3:30 usiku, ICU; Ijumaa saa 1:00 usiku, Mizani ya Ushambenga; kila Jumatano,

Huba; Jumatatu hadi Ijumaa saa 3:00 usiku na Harusi Yetu; Alhamisi saa 1:00 usiku.

## Daraja la Kwanza Z'bar kurindima leo

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

LIGI Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, inatarajia kuanza kutimua vumbi katika viwanja mbalimbali vya Kisiwani Unguja leo ambapo African Coast itaumana na Bridge Star katika Uwanja wa Cairo wakati Dulla Boys wakiwa na kazi ngumu dhidi ya Chuoni kwenye Dimba la Kitogani.

Timu zingine zitakazoshuka dimbani leo ni New King dhidi ya New Power katika Uwanja wa Kinyasini wakati Dimba la Amaan, Kilimani City itakuwa ikivaana na Kundemba.

Ligi hiyo yenye jumla ya timu 16 msimu huu, mbili zitapanda daraja kucheza Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao na nne za mwisho zitashuka daraja na kurudi katika ligi za mikoa zilipotoka.

Akizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Ligi Zanzibar (ZLB), Sheha Mohmed, alisema ratiba ya ligi hiyo tayari imeshatolewa kwa klabu zote na maandalizi yote yamekamilika huku jumla ya viwanja sita vikitarajiwa kutumika kuchezewa ligi hiyo.

Alivitaja viwanja hivyo kwa upande wa Kaskazini ni Kinyasini na Cairo huku Mkoa wa Kusini Unguja vikiwa ni Mchangani na Kitogani wakati Mkoa wa Mjini Magharibi akivitaja kuwa ni Ngome, Amaan, Mau A na Mau B.

## Dodoma Jiji nayo yaja na tuzo mchezaji bora

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Dodoma Jiji imeanzisha tuzo ya mashabiki wao kwa kila mwezi kama ambavyo wanafanya mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba, huku mchezaji Aboukakae Ngalema akiibuka kuwa mchezaji bora wa mwezi Oktoba.

Hafla hiyo ilifanyika juzi, ikiambatana na uzinduzi wa Tawi la Marafiki wenye hadhi ya juu liitwalo 'Friends of DJFC-VIP' lililopo jijini Dodoma.

Mtandao wa Instagram wa klabu hiyo, umeeleza Mkuu wa Mkoa wa Dodoma na mlezi wa timu hiyo, Antony Mavunde, ndiye aliyekuwa mgeni rasmi ya shughuli hizo, na kumkabidhi mchezaji huyo tuzo.

"Aboubakar Ngalema ameibuka mchezaji bora wa mwezi katika tuzo iliyotolewa na mashabiki wa 'Friends of DJFC-VIP', katika halfa iliyoambatana na uzinduzi wa tawi hilo. Tuzo hiyo ilikabidhiwa na mlezi na timu yetu, Antony Mavunde, ambaye alikuwa mgeni rasmi," uliandika mtandao wa klabu hiyo.

Kwa sasa Dodoma Jiji inajiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Biashara United itakayopigwa Jumapili wiki hii katika uwanja wao wa nyumbani wa Jamhuri.

## ZISIKUPITE

### BARCA YATAKA WA3 CHELSEA

BARCELONA wanapanga kuwasajili wachezaji watatu wa Chelsea - kiungo wa Morocco, Hakim Ziyech miaka 28, winga wa England, Callum Hudson-Odoi miaka 21, na kiungo wa Marekani, Christian Pulisic miaka 23. **(Catalan Daily Sport, via AS)**

### ZIYECH ATAKIWA DORTMUND

KLABU ya Borussia Dortmund pia inavutiwa na Hakim Ziyech wa Chelsea na wamekuwa wakiwasiliana na kambi ya mchezaji huyo. **(Bild, via Inside Futbol)**

### CONTE NA MAN UNITED

MANCHESTER United iliachana na mpango wa kumleta kocha anayeinoa Tottenham Hotspur kwa sasa, Antonio Conte kwa sababu raia huyo wa Italia kutaka bajeti kubwa ya kiasi cha pauni milioni 250 kwa ajili ya usajili. **(90min)**

### ZIDANE KUMRITHI SOLSKJAER

MANCHESTER United wanamatumaini ukaribu wa Zinedine Zidane na Cristiano Ronaldo na Raphael Varane unaweza kumshawishi kujiunga na klabu hiyo na kuwa mbadala wa Ole Gunnar Solskjaer, kama atatimuliwa. **(Mirror)**

### SPURS, CITY ZAITIWA VLAHOVIC

TOTTENHAM Hotspur na Manchester City zimefahamishwa kwamba zinaweza kumsajili mshambuliaji wa Fiorentina na Serbia, Dusan Vlahovic mwenye umri wa miaka 21 katika dirisha la Januari, lakini kama watalipa pauni milioni 70. **(Sun)**

### DE BEEK KUONDOKA JANUARI

KIUNGO wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 24, ameamua ataondoka Manchester United, Januari. **(Metro)**

### HENDERSON KURUHUSIWA KUONDOKA

KLABU ya Manchester United itamruhusu kipa wake, Dean Henderson mwenye umri wa miaka 24, kuondoka kwa mkopo wa miezi 18 Januari. **(Sun)**

### RABIOT ANYATIWA NEWCASTLE

KIUNGO wa Juventus na Ufaransa, Adrien Rabiot mwenye umri wa miaka 26, ananyatiwa na Newcastle United. **(Calciomercato)**

### INSIGNE ATAKIWA CHELSEA

CHELSEA inamfuatilia mshambuliaji wa Napoli na Italia, Lorenzo Insigne mwenye umri wa miaka 30. **(Marca)**

### TCHOUAMENI AGOMBEWA

REAL Madrid itapambana na Chelsea katika mbio za kumsajili kiungo wa Monaco na Ufaransa, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 21. **(Marca)**

### BALOGUN ASAKWA MIDDLESBROUGH

MSHAMBULIAJI wa Arsenal na Timu ya Taifa ya England, Folarin Balogun mwenye umri wa miaka 20, anasakwa na Middlesbrough. **(Sun)**



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# RONALDO HATARINI KUKOSA KOMBE LA DUNIA QATAR

**●●●Serbia yaiweka matatani ikifuzu kutoka Kundi A, sasa Ureno yasubiri mechi za mtoano za washindi wa pili wa...**

**LISBON, Ureno**

MATUMAINI ya Cristiano Ronaldo na timu yake ya taifa kufuzu Kombe la Dunia mwaka 2022 yapo shakani baada ya Serbia kutoka nyuma na kushinda 2-1 dhidi ya Ureno na kufuzu kwenye Kundi lao A, Jumapili.

Bao la kichwa la dakika ya 90 la Aleksandar Mitrovic aliyetokea benchi liliiwezesha Serbia kupaa kileleni mwa kundi na kufikisha pointi 20, tatu zaidi ya Ureno inayoshika nafasi ya pili, ambayo ilihitaji sare tu kumaliza kileleni na kufuzu kwa tofauti ya mabao.

Badala yake Ronaldo na Ureno watasubiri mechi za mtoano za washindi wa pili wa kila kundi kuweza kufuzu kucheza Kombe la Dunia Qatar 2022.

Mitrovic alimfunga golikipa, Rui Patricio kwa mpira wa kichwa na kuamsha shangwe kwenye benchi la Serbia, baada ya nahodha Dusan Tadic kusawazisha lile la ufunguzi la Ureno lililofungwa na Renato Sanches mapema.

Mashabiki walijazana katikati ya Jiji la Belgrade nchini Serbia kushangilia furaha hiyo wakiwa na bendera ya nchi yao, wakati vijana wao wakifuzu moja kwa moja kule Ureno.

Hukuwa nahodha wa Ureno, Ronaldo akionekana kutokuwa na makali yake, kiungo Joao Palhinha alisema hawakucheza vizuri.

"Tunatakiwa kukubali matokeo, tulikuwa na mchezo mbaya," alisema Palhinha akiiambia televisheni ya Taifa ya Ureno, RTP.

"Tulijilinda sana kipindi cha pili. Lazima tuwasifie Serbia, walicheza vizuri sana, na walistahili ushindi."

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS.686

MECHI KALI
HOME AWAY
WALES
3.15 | 3.30 | 2.28
BELGIUM

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa
halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LLORIS HAJUI HATIMA YAKE TOTTENHAM



**PARIS, Ufaransa**

HUGO Lloris anapanga kufanya mazungumzo na Tottenham Hotspur kuhusu majaliwa yake baada ya Juni, huku akiacha mlango wazi kurudi kwenye Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Mkataba wa Lloris na Spurs unamalizika Juni 30, mwakani na majaliwa ya golikipa huyo mwenye umri wa miaka 34, ambaye alijiunga na klabu hiyo mwaka 2012 bado hayajulikani.

Taarifa zaidi zinasema kwamba, golikipa huyo anaweza kuondoka kule London Kaskazini na kurudi Ufaransa ambako alicheza awali katika Klabu za Nice na Lyon.

Kwa sasa Lloris ana matumaini ya kubeba taji na kocha mpya Antonio Conte wakati wakijiweka kwenye nafasi ya kubeba kombe la kwanza kwa kipindi cha miaka 13.

"Sijafunga milango," alisema Lloris Jumapili, wakati alipoulizwa kama atarudi kwenye soka la Ufaransa.

"Kwa sasa nafasi ya kwanza naipa Spurs. Bado tunapambania taji. Nataka kusaidia maendeleo ya klabu.

"Tayari tumepata uzoefu wa vitu vikubwa na mashabiki wetu, kwa sasa nataka kuwa mtulivu."

Katika Jarida la L'Equipe, Lloris alinukuliwa akisema: "Tutakuwa na mazungumzo wiki chache zinazokuja. Na kwa sasa najaribu kuzoea kile ambacho kinatakiwa na kocha mpya, Antonio Conte. Kwani bado kuna presha kubwa."

Lloris na mabingwa watetezi wa Kombe la Dunia Ufaransa wameshafuzu kucheza Kombe la Dunia mwaka ncini Qatar baada ya kuwafunga mabao 8-0 Kazakhstan Jumamosi, ambapo Kylian Mbappe alifunga manne, na leo Jumanne watacheza na Finland kwenye mchezo wao wa mwisho wa kundi.

# Xavi kuchota nyota watatu Chelsea



**BARCELONA, Hispania**

KOCHA Mkuu wa Barcelona, Xavi Hernandez, anataka kukijenga upya kikosi chake baada ya kuchukua mikoba ya Ronald Koeman, huku jicho lake akilielekeza kwa nyota wa Chelsea, kwa mujibu wa ripoti.

Dirisha dogo la usajili la Januari litakuwa bize kwa Xavi na Barcelona wakiripotiwa kuhitaji huduma za wachezaji wa Chelsea, Hakim Ziyech, Christian Pulisic na Callum Hudson-Odoi.

Kwa mujibu wa Diario Sport, Barcelona inatarajia kuwasajili wachezaji hao watatu ambao wamekuwa wakipambana kupata muda wa kucheza chini ya kocha, Thomas Tuchel na wanaonekana watakuwa wazuri katika eneo la ushambuliaji kwenye kikosi cha Xavi.

Xavi tayari amemleta mchezaji mwenzake wa zamani, Dani Alves katika kikosi chake pia amehusishwa kumleta Camp Nou mchezaji wa zamani wa Barca na sasa Liverpool, Thiago Alcantara.

Ripoti hiyo imesema kwamba, Rais wa Barcelona, Joan Laporta yupo tayari kumpa kitita chochote atakachokitaka ili kukamilisha zoezi hilo la kuimarisha timu.

Hata hivyo, Barca wanakabiliwa na ukata wa kifedha na usaji wa Januari utakuwa ule wa kuwachukua wachezaji kwa mkopo.

## HABARI MICHEZO

# 6,934,380

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 20.11.21 | 18:00 | Burnley vs Crystal Palace | 2.80 | 3.21 | 2.55 |
| 2. 20.11.21 | 18:00 | Aston Villa vs Brighton | 2.50 | 3.25 | 2.85 |
| 3. 20.11.21 | 18:00 | Newcastle vs Brentford | 2.69 | 3.24 | 2.64 |
| 4.20.11.21 | 18:00 | Wolverhampton vs West Ham | 3.01 | 3.21 | 2.41 |
| 5. 20.11.21 | 18:00 | Hull City vs Birmingham | 2.63 | 3.12 | 2.63 |
| 6. 20.11.21 | 18:00 | Reading vs Nottingham | 2.89 | 3.18 | 2.39 |
| 7. 20.11.21 | 20:00 | Lazio vs Juventus | 2.78 | 3.36 | 2.48 |
| 8. 20.11.21 | 20:45 | Sparta Rotterdam vs Twente | 2.61 | 3.20 | 2.61 |
| 9. 20.11.21 | 22:45 | Fiorentina vs AC Milan | 3.09 | 3.39 | 2.26 |
| 10. 21.11.21 | 15:00 | Brest vs Lens | 3.03 | 3.43 | 2.26 |
| 11. 21.11.21 | 17:00 | Salernitana vs Sampdoria | 3.00 | 3.29 | 2.37 |
| 12. 21.11.21 | 17:00 | Troyes vs St Etienne | 2.35 | 3.34 | 2.94 |
| 13. 21.11.21 | 17:00 | Metz vs Bordeaux | 2.42 | 3.28 | 2.88 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 16 - NOVEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 1525 | Vietnam vs Saudi Arabia | 7.11 | 4.32 | 1.37 |
| 15:00 | 1921 | Lebanon vs United Arab Emirates | 3.33 | 2.94 | 2.18 |
| 16:00 | 2424 | Egypt vs Gabon | 1.40 | 3.96 | 7.53 |
| 16:00 | 2662 | Mozambique vs Malawi | 2.78 | 2.88 | 2.54 |
| 16:00 | 5163 | Libya vs Angola | 2.34 | 2.88 | 3.08 |
| 17:00 | 1985 | Liechtenstein U21 vs Belarus U21 | 43.29 | 17.32 | 1.01 |
| 17:00 | 2770 | Greece U21 vs Iceland U21 | 1.75 | 3.65 | 3.94 |
| 18:00 | 4783 | Iraq vs South Korea | 5.20 | 3.37 | 1.64 |
| 18:00 | 4839 | China vs Australia | 8.48 | 4.15 | 1.35 |
| 19:00 | 1429 | Liberia vs Central African Republic | 2.75 | 2.84 | 2.60 |
| 19:00 | 1548 | Azerbaijan U21 vs Norway U21 | 7.70 | 4.72 | 1.32 |
| 19:00 | 2358 | Syrian Arab Republic vs Iran | 7.32 | 3.75 | 1.43 |
| 19:00 | 2513 | Wales U21 vs Switzerland U21 | 3.56 | 3.61 | 1.85 |
| 19:00 | 2700 | Ukraine U21 vs Serbia U21 | 1.73 | 3.56 | 4.14 |
| 19:00 | 3938 | Nigeria vs Cape Verde | 1.45 | 3.80 | 6.73 |
| 19:00 | 4060 | Bosnia and Herzegovina U21 vs Montenegro U21 | 1.98 | 3.38 | 3.34 |
| 19:00 | 4140 | Oman vs Japan | 7.52 | 4.05 | 1.39 |
| 19:00 | 4479 | Algeria vs Burkina Faso | 1.28 | 4.43 | 10.60 |
| 19:30 | 2906 | Lithuania U21 vs Slovakia U21 | 4.23 | 3.80 | 1.66 |
| 19:30 | 5358 | Bulgaria U21 vs Moldova U21 | 1.43 | 4.33 | 5.97 |
| 19:30 | 5485 | Poland U21 vs Latvia U21 | 1.11 | 6.95 | 18.33 |
| 20:00 | 1144 | Slovenia U21 vs Czech Republic U21 | 2.84 | 3.32 | 2.24 |
| 20:00 | 2683 | Turkey U21 vs Denmark U21 | 2.99 | 3.33 | 2.15 |
| 20:00 | 5007 | Russia U21 vs Spain U21 | 5.01 | 4.43 | 1.48 |
| 20:30 | 4012 | Macedonia U21 vs France U21 | 10.57 | 5.57 | 1.21 |
| 20:40 | 5124 | Israel U21 vs Hungary U21 | 1.69 | 3.76 | 4.15 |
| 21:00 | 4666 | Kosovo U21 vs Albania U21 | 3.09 | 3.38 | 2.08 |
| 22:00 | 3155 | Morocco vs Guinea | 1.32 | 4.23 | 9.61 |
| 22:00 | 4308 | Ireland U21 vs Sweden U21 | 2.93 | 3.37 | 2.16 |
| 22:00 | 4744 | Mauritania vs Equatorial Guinea | 3.95 | 3.18 | 1.88 |
| 22:00 | 5647 | Cameroon vs Ivory Coast | 2.16 | 2.93 | 3.37 |
| 22:05 | 1343 | Scotland U21 vs Belgium U21 | 3.81 | 3.72 | 1.76 |
| 22:15 | 5343 | Portugal U21 vs Cyprus U21 | 1.01 | 12.51 | 48.11 |
| 22:30 | 1845 | Northern Ireland U21 vs Malta U21 | 1.24 | 5.41 | 9.46 |
| 22:30 | 3962 | Austria U21 vs Croatia U21 | 2.50 | 3.26 | 2.54 |
| 22:45 | 1009 | Czech Republic vs Estonia | 1.12 | 8.57 | 20.94 |
| 22:45 | 1015 | Bosnia and Herzegovina vs Ukraine | 4.31 | 3.66 | 1.80 |
| 22:45 | 1446 | Finland vs France | 5.01 | 3.81 | 1.67 |
| 22:45 | 1523 | Cambridge Utd vs Northampton | 2.20 | 3.35 | 3.10 |
| 22:45 | 1948 | Oldham vs Ipswich | 4.26 | 3.76 | 1.74 |
| 22:45 | 2030 | Notts County vs Rochdale | 2.45 | 3.41 | 2.67 |
| 22:45 | 3230 | Wales vs Belgium | 3.15 | 3.30 | 2.28 |
| 22:45 | 3279 | Stevenage vs MK Dons | 3.36 | 3.51 | 2.03 |
| 22:45 | 3883 | Montenegro vs Turkey | 5.03 | 3.77 | 1.68 |
| 22:45 | 3893 | Plymouth vs Sheffield Wed | 2.34 | 3.35 | 2.86 |
| 22:45 | 5017 | Gibraltar vs Latvia | 8.21 | 4.91 | 1.36 |
| 22:45 | 5544 | Netherlands vs Norway | 1.45 | 4.69 | 6.39 |
| 22:45 | 5702 | Carrick Rangers vs Crusaders Belfast | 4.63 | 4.15 | 1.55 |
| 22:45 | 5729 | Exeter vs Bradford City | 2.18 | 3.40 | 3.11 |
| 23:00 | 4292 | Bolivia vs Uruguay | 3.35 | 3.30 | 2.18 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.




# ABRAHAM AFUNGUKA MOURINHO KUMPAISHA

**LONDON, England**

MSHAMBULIAJI wa AS Roma, Tammy Abraham, ameelezea siri ya kuwa imara uwanjani aliyofundishwa na kocha wake wa sasa, Jose Mourinho.

Abraham amebainisha kwamba, Mourinho amemjengea ujasiri na kumrudisha katika makali yake hali iliyomfanya aitwe tena kikosi cha Timu ya Taifa ya England.

Nyota huyo ambaye alianzia maisha yake ya soka kwenye akademi ya Chelsea hadi alipopandishwa timu ya wakubwa na baada ya kutokupata nafasi ya kucheza mara kwa mara akapelekwa kwa mkopo kwenda klabu za Bristol City, Swansea City, Aston Villa na kurudi tena Stamford Bridge kabla ya kuuzwa kwenda Roma.

Alipoulizwa ni kwa kiasi gani Mourinho amemsaidia, alijibu ni, "kuwa mnyama kweli", nafikiria kitu kimoja alichoniambia, nilikuwa laini laini na nahitaji kuwa mtu wa nguvu kama mshambuliaji."

"Si suala la kuwa laini kwenye uwanja, unahitaji kuwa mtu wa nguvu, ili uwapo wako uwaogopeshe mabeki, nadhani hicho ndicho nilichojifunza na naendelea kukifanyia kazi," aliongezea Abraham.

Abraham kwa sasa ameitwa tena kwenye kikosi cha England katika michuano ya kufuzu Kombe la Dunia nchini Qatar 2022.

Alisajiliwa Roma akitokea Chelsea kwa ada ya pauni milioni 34 na kusaini mkataba wa miaka mitano, huku pia kukiwa na kipengele cha Chelsea kuweza kumnunua tena kwa kiasi cha pauni milioni 68, lakini lazima awe amecheza misimu miwili.

# Donnarumma mambo bado magumu PSG



**PARIS, Ufaransa**

GOLIKIPA namba mbili wa Klabu ya Paris Saint-Germain, Gianluigi Donnarumma ameweka wazi kwamba, hajazoea hali ya kushindania namba na mchezaji mwingine.

Donnarumma alijiunga na PSG akitokea AC Milan kama mchezaji huru baada ya mkataba wake na klabu hiyo kumalizika mwishoni mwa msimu wa 2020/2021 na kuamua kutafuta changamoto mpya.

Kipa huyo ameshindwa kuchukua nafasi ya Keylor Navas ambaye amekuwa kipa namba moja wa PSG tangu ajiunge na miamba hiyo ya Ufaransa akitokea Real Madrid.

"Haiathiri kiwango changu, lakini inanisumbua," Donnarumma aliiambia TNT Sport katika mahojiano kuhusu upinzani wa namba dhidi ya Navas.

"Si rahisi, kwa sababu siku zote nimezoea kuwa namba moja na muda mwingine inauma kukaa benchi.

"Lakini nina hakika jambo hili litamalizwa," aliongeza.

# Michezo

Jumanne Novemba 16, 2021

Nipashe




**Ronaldo hatarini kukosa Kombe la Dunia Qatar**

UKURASA 21

MABINGWA...




Timu ya mpira wa Kikapu ya Wanawake Mkoa wa Dar es Salaam, wakifurahia kuibuka mabingwa baada ya kukabidhiwa kombe na mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 6.5 kwa kuibuka mabingwa wa mashindano ya CRDB Bank Taifa Cup 2021 yaliyofikia kilele chake mwishoni mwa wiki jijini Dodoma katika viwanja vya Chinangali Park.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# PABLO, NABI MAPEMA TU MOTO SIMBA, YANGA

● ● ● Wawahisha vikosi kambini kuzitafutia kwanza kasi Ruvu Shooting na Namungo kabla ya...

**Na Saada Akida**

MAKOCHA wa vigogo vya soka nchini, Simba na Yanga wamewasha moto mapema kila mmoja akitaka kuhakikisha hapotezi alama tatu kuelekea mechi zao za Ligi Kuu Bara wiki hii, wakati watakapoziongoza timu zao kwenye viwanja tofauti Ijumaa na Jumamosi.

Simba ambayo inashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu, Ijumaa itashuka katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza kuivaa Ruvu Shooting wakati vinara wa ligi hiyo, Yanga wenyewe wakiwa na shughuli pevu Jumamosi katika Uwanja wa Ilulu mkoani Lindi dhidi ya wenyeji wao, Namungo FC.

Kuelekea mechi hizo, tayari makocha wa vigogo hivyo vya soka nchini, Mhispania Pablo Franco wa Simba na Mtunisia Nasreddine Nabi wa Yanga, wamevitaka vikosi vyao kuingia kambini mara moja kuanza maandalizi ya kusaka alama hizo tatu muhimu.

Hii itakuwa mara ya kwanza kwa Kocha Mkuu wa Simba, Pablo kuiongoza timu hiyo kwenye mechi ya Ligi Kuu na tayari tangu jana jioni kikosi cha timu hiyo kimeingia kambini kujiwinda na mchezo huo.

"Kikosi chetu kitaingia kambini leo baada ya mazoezi ya jioni kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu ya NBC dhidi ya Ruvu Shooting utakaopigwa Novemba 19, katika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

"Wachezaji waliokuwa katika kikosi cha timu ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars) kilichocheza jana (juzi) dhidi ya Madagascar nao ni miongoni mwa watakaoingia kambini," ilieleza taarifa ya Simba.

Aidha, taarifa hiyo imeeleza kuwa nyota watatu; Mzambia Rally Bwalya na Wamalawi Duncan Nyoni na Peter Banda wao hawatakuwa sehemu ya wachezaji waliotarajiwa kuingia kambini jana kutokana na majukumu yao ya timu zao za taifa na watatua nchini baada michezo hiyo itakayopigwa leo. Bwalya leo anatarajiwa kuwa sehemu ya kikosi cha Zambia kitakachoshuka dimbani ugenini dhidi ya Tunisia kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar, wakati Nyoni na Banda nao wakiwa na jukumu kama hilo ugenini dhidi ya Msumbiji.

Kwa upande wa Yanga, uongozi wa klabu hiyo umesema leo kikosi chao kitaingia kambini rasmi kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wao wa Jumamosi dhidi ya Namungo.

Yanga waliweka kambi ya siku saba visiwani Zanzibar kwa wachezaji ambao hawako katika timu za taifa na kucheza mechi mbili za kirafiki dhidi ya Mlandege na KMKM, ikiwa ni maandalizi ya michezo iliyopo mbele yao.

Akizungumza jijini jana, Nabi alisema baada ya Jumamosi kurejea wachezaji walipewa mapumziko ya siku mbili na kesho (leo), wanarudi kambini wachezaji wote kuhakikisha wanajipanga vizuri kuelekea mchezo dhidi ya Namungo.

"Tulikuwa na wakati mzuri Zanzibar, tumepata nafasi ya kupanga mambo yetu, licha ya ushindi tuliopata visiwani humo katika michezo yetu miwili, lakini kuna mambo mengi tumeweza kuyaboresha pamoja na kuwa na wachezaji wachache.

"Hatuna mechi iliyokuwa rahisi kwetu, tumewaona Namungo FC wanavyocheza tumeanza kufanyia kazi mapungufu yetu na ubora wa Namungo FC, kuhakikisha tunaendelea kupata matokeo chanya na kufikia malengo yanayotarajiwa ya kutwaa ubingwa," alisema Nabi.

Nyota wa Yanga ambao wako katika timu za taifa ni Khalid Aucho (Uganda), kipa Djigui Diarra (Mali), Ramadhan Kabwili, Kibwana Shomari, Dickson Job, Bakari Mwamnyeto, Zawadi Mauya, Feisal Salum (wote Tanzania) na Djuma Shaban (DR Congo).

## Samatta na simulizi ya wanajeshi kumvamia

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI nahodha wa Tanzania, Taifa Stars, Mbwana Samatta akisema kuwa kuzuiwa kwao ofisini na wanajeshi wa Madagascar ilikuwa ni figisu na wala si kweli kama walikuwa na maambukizo ya virusi vya corona, Simon Msuva amesema iwapo timu hiyo itakuwa na wachezaji 10 tu wanaocheza soka la kulipwa nje, basi itafika mbali.

Wakizungumza baada ya kutoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Madagascar jijini Antananarivo, Samatta alisema ni kweli yeye na wenzake Aishi Manula na Bakari Mwamnyeto waliambiwa kuwa wana maambukizi ya virusi vya corona, lakini anashangaa kuona wakati wa kuondoka waliruhusiwa kuondoka.

"Walisema tuna corona, lakini ninavyojua mtu anayepata maambukizi hayo haruhusiwi kutoka ndani ya nchi aliyokuwapo, lakini sisi tuliruhusiwa kuondoka, sijui kwa nini, lakini wengi wanasema waliamua tu kufanya mchezo mchafu," alisema nahodha huyo huku akifafanua kuwa kwenye soka la Afrika, hivyo ni viti vya kawaida na wala si vigeni.

"Vitu hivi kwenye soka la Afrika ni vya kawaida, vinajulikana na vipo, ila tu kwetu inaweza kuwa fundisho pia," alisema.

Kwa upande wa Msuva aliyeweka rekodi ya kuzifunga timu zote kwenye Kundi J, kusaka tiketi ya kufuzu kucheza Kombe la Dunia nchini Qatar mwakani, amesema kama Tanzania itapata wachezaji 10 ambao wanacheza nje ya nchi, itakuwa timu bora na yenye uwezo wa kufika mbali kwenye michuano yoyote Afrika.

"Kuwakosa wachezaji wenzetu muhimu ilituathiri sana kwa sababu ni tegemeo, lakini kocha akaona ana wachezaji wengi, akawapa nafasi wengine na wameonyesha kitu, ila kwa hili lililotokea kuna kitu cha kujifunza kwa sisi Watanzania. Pia ninachoona karibuni kila mechi wachezaji wa Tanzania tunabadilika na kuwa wazuri zaidi, ila tusiishie hapa, naomba tu tusiwe sisi tu ndiyo wachezaji wa kutoka nje ya nchi, naomba kuwe na wachezaji 10 wa nje ya nchi, nina uhakika tutafika mbali sana," alisema Msuva.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >